



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**



## MWONGOZO WA UPIMAJI KATIKA SHULE ZA MSINGI

Umeandaliwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania  
S.L.P 2624,  
Dar es salaam, Tanzania.

Agosti, 2022



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



### **MWONGOZO WA UPIMAJI KATIKA SHULE ZA MSINGI**

*Umeandaliwa na*

Baraza la Mitihani la Tanzania  
S.L.P 2624,  
Dar es salaam, Tanzania.

Agosti, 2022

Baraza la Mitihani la Tanzania  
S.L.P 2624,  
Dar es salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2022

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

1.0	UTANGULIZI .....	1
2.0	MAANA YA UPIMAJI, MALENGO NA AINA ZA UPIMAJI.....	1
2.1	Upimaji.....	1
2.2	Malengo ya Upimaji.....	2
2.3	Aina za Upimaji.....	3
2.3.1	Upimaji wa Awali (Placement Assessment).....	3
2.3.2	Upimaji Endelevu (Formative Assessment) .....	3
2.3.3	Upimaji Tatuzi/Gunduzi (Diagnostic Assessment).....	4
2.3.4	Upimaji Tamati (Summative Assessment).....	4
3.0	UTHABITI NA KUAMINIKA KWA JARIBIO.....	5
3.1	Uthabiti wa Jaribio (Reliability of a Test).....	5
3.1.1	Mambo yanayoathiri Uthabiti wa Jaribio .....	5
3.2	Kuaminika kwa Jaribio (Validity of a Test).....	6
3.2.1	Mambo Yanayoathiri Kuaminika kwa Jaribio .....	6
3.3	Hatua za Kutunga Maswali Bora ya Upimaji.....	9
3.4	Upimaji Unaozingatia Umahiri.....	10
4.0	TAKSONOMIA YA BLOOM .....	14
4.1	Nyanja ya Utambuzi (Cognitive Domain) .....	14
4.2	Nyanja ya Mwelekeo (Affective Domain) .....	14
4.3	Nyanja ya Stadi (Psychomotor Domain) .....	14
4.4	Umuhimu wa Taksonomia ya Bloom.....	15
5.0	HATUA ZA KUANDAA MTIHANI/JARIBIO .....	20

5.1	Utayarishaji wa Jedwali la Utahini.....	20
5.2	Malengo ya Kuandaa Jedwali la Utahini .....	20
5.3	Mambo Muhimu ya Kuzingatia Wakati wa Kuandaa Jedwali la kutahini. ....	21
5.4	Hatua za Kuandaa Jedwali la Kutahini.....	21
6.0	UTUNGAJI WA MASWALI YA MTIHANI/JARIBIO .....	25
6.1	Aina za Maswali.....	26
6.1.1	Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi .....	27
6.1.1.1	Manufaa ya Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi.....	29
6.1.1.2	Udhaifu wa Maswali ya Kuchagua .....	29
6.1.1.3	Misingi ya Utungaji wa Maswali ya Kuchagua Jibu .....	30
6.1.2	Maswali ya Kuoanisha .....	39
6.1.2.1	Manufaa ya Maswali ya Kuoanisha .....	39
6.1.2.2	Udhaifu wa Maswali ya Kuoanisha .....	39
6.1.2.3	Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Kuoanisha.....	40
6.1.3	Maswali ya Kweli/Si kweli .....	44
6.1.3.1	Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Kweli/Si kweli .....	46
6.1.4	Maswali ya Majibu Mafupi .....	50
6.1.4.1	Makundi ya Maswali ya Majibu Mafupi .....	50
	Katika ngazi ya Elimu Msingi aina ya maswali ya majibu mafupi yanayotumika zaidi katika kundi hili ni:.....	50
6.1.4.2	Manufaa ya Maswali ya Majibu Mafupi.....	53
6.1.4.3	Udhaifu wa Maswali ya Majibu Mafupi.....	54

6.1.4.4	Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Majibu Mafupi .....	54
6.1.4.5	Aina za Maswali ya Majibu Mafupi (Objective Questions).....	56
7.0	MWONGOZO WA USAHIHISHAJI.....	59
7.1	Mambo ya Kuzingatia Katika Kuandaa Mwongozo wa Usahihishaji.....	59
8.0	UREKEBISHAJI WA MASWALI YA UPIMAJI/MITIHANI.....	60
9.0	UENDESHAJI WA UPIMAJI .....	61
9.1	Majukumu ya Msimamizi Kabla ya Upimaji Kufanyika.....	62
9.2	Majukumu ya Msimamizi Wakati wa Ufanyikaji wa Upimaji.....	63
9.3	Majukumu ya Msimamizi Baada ya Upimaji Kufanyika .....	64
10.0	USAHIHISHAJI WA UPIMAJI.....	65
11.0	KUREKODI ALAMA ZA UPIMAJI .....	66
12.0	UPIMAJI WA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM .....	67
13.0	UFUATILIAJI NA TATHMINI.....	72
14.0	HITIMISHO.....	73

## **ORODHA YA MAJEDWALI**

Jedwali Na 1: Sampuli ya Maswali yanayopima Umahiri Ikilinganishwa na Maswali Yanayopima Uwezo wa Kukariri .....	11
Jedwali Na. 2: Taksonomia Iliyoboreshwa na ya Zamani.....	15
Jedwali Na. 3: Vitenzi na Sampuli ya Maswali yanayotumika katika Ngazi mbalimbali za Taksonomia ya Bloom .....	16
Jedwali Na. 4: Umahiri Ulifundishwa na Muda Uliotumika katika Ufundishaji Somo la Kiswahili .....	22
Jedwali Na. 5: Uzito wa kila Umahiri .....	23
Jedwali Na. 6: Idadi ya Maswali katika Kila Umahiri.....	24
Jedwali Na. 7: Mfano wa Jedwali la Utahini katika Somo la Kiswahili .....	25
Jedwali Na 8: Mfano wa Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Wanafunzi Wasioona .....	68

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania ni Taasisi ya serikali chini ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ilioanzishwa mwaka 1973 kwa sheria ya Baraza la Mitihani la Tanzania sura ya 107 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019. Pamoja na majukumu mengine, Baraza la Mitihani la Tanzania limepeewa jukumu la kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) na Upimaji ngazi ya Elimu ya Msingi. Lengo la kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi ni pamoja na kuchagua wanafunzi wenyewe sifa za kuendelea na masomo ya sekondari pamoja na vyuo vya kati. Aidha, huendesha Upimaji wa Darasa la Nne kwa lengo la kuwabaini wanafunzi waliopata stadi za kuwawezesha kuendelea masomo ya Darasa la Tano (waliomudu stadi za juu za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu). Kutokana na majukumu hayo Baraza la Mitihani la Tanzania limeona kuna umuhimu wa kuandaa mwongozo utakaowawezesha walimu wa shule za msingi kuboresha namna ya kufanya upimaji wa maendeleo ya wanafunzi ili kupata matokeo yanayoakisi uhalisia wa uwezo wa wanafunzi hao.

Mwongozo huu unaelezea dhana ya upimaji, malengo ya upimaji, aina za upimaji na hatua mbalimbali za upimaji, ikiwa ni pamoja na uandaaji wa jedwali la upimaji. Vile vile, mwongozo umeeleza namna bora ya urekebishaji wa maswali, uendeshaji wa upimaji na usahihishaji. Pia mwongozo umeeleza namna bora ya utunzaji wa alama zinazotokana na upimaji kwa matumizi mbalimbali ikiwemo uboreshaji wa ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mwongozo huu unaelekeza namna ya kuandaa upimaji na kufanya ufuatiliaji.

Baraza la Mitihani linatarajia kuwa, mwongozo huu utakuwa chachu kwa wadau wote wa elimu, hususan walimu wa shule za msingi katika kuandaa maswali bora ya upimaji wa wanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwongozo pia utasaidia Wathibiti Ubora wa Shule katika kufuatilia na kufanya tathmini kuhusu umahiri wa walimu katika kuwapima wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Baraza la Mitihani linawashukuru wote walioshiriki katika kuandaa mwongozo huu.



Athuman S. Amasi

## KAIMU KATIBU MTENDAJI

## **1.0 UTANGULIZI**

Mwongozo huu wa upimaji umeandaliwa kwa lengo la kuwajengeta uwezo walimu wanaofundisha Shule za Msingi kuhusu namna ya kuboresha upimaji katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwongozo huu unaonesha namna upimaji wa maendeleo ya wanafunzi unavyotakiwa kufanyika ili kupata matokeo yanayoakisi uwezo halisi wa mwanafunzi. Aidha, unaelezea dhana ya upimaji, malengo, aina na hatua za upimaji. Pia unaeleza namna bora ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya upimaji. Vile vile mwongozo unafafanua misingi ya uandaaji wa maswali bora ya upimaji na ufanyikaji wa upimaji. Zaidi ya hayo, mwongozo umebainisha mbinu za usahihishaji wa upimaji na utunzaji wa alama za wanafunzi zinazotokana na upimaji/mtihani husika.

Kwa kuzingatia vigezo vyta upimaji vilivyobainishwa katika mwongozo huu, mwalimu atawezekana kufanya upimaji kwa kutumia vigezo stahiki vitakavyomsaidia kupata matokeo yanayoendana na uwezo wa kila mwanafunzi. Vigezo hivyo ni kama vile; kuandaa jedwali la upimaji, kutunga aina mbalimbali za maswali yenye ubora unaolingana na ngazi ya elimu ya Msingi, kuendesha na kusahihisha upimaji kwa kufuata utaratibu unaotakiwa pamoja na kurekodi na kutunza alama za matokeo ya upimaji wa somo husika.

## **2.0 MAANA YA UPIMAJI, MALENGO NA AINA ZA UPIMAJI**

### **2.1 Upimaji**

Upimaji katika elimu ni kitendo endelevu cha kutafuta ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa au stadi zilizofundishwa kwa kuzingatia malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa vipengele mbalimbali vyta umahiri kama vilivyobainishwa kwenye muhtasari wa somo husika. Pia, upimaji hujumuisha mwenendo, tabia na uwezo wa mwanafunzi wa kufanya mambo mbalimbali.

## **2.2 Malengo ya Upimaji**

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hauwezi kukamilika bila kufanya upimaji. Upimaji hufanyika ili:

- (i) kubaini kiwango cha uelewa kilichofikiwa na wanafunzi baada ya kufundishwa na kujifunza maudhui/mada mbalimbali;
- (ii) kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo ya upimaji humsaidia mwalimu kuboresha mbinu, njia na zana anazotumia katika ufundishaji iwapo wanafunzi wake watakuwa wamepata ufaulu wa chini. Aidha, wanafunzi wataona umuhimu wa kuongeza juhudi katika ujifunzaji;
- (iii) kubaini matatizo ya mwanafunzi katika kujifunza. Matokeo ya upimaji humsaidia mwalimu kufanya uchunguzi yakinifu na kubaini changamoto inayosababisha wanafunzi kufanya vibaya, hatimaye kugundua tatizo na kulitafutia ufumbuzi. Kwa hiyo kutokana na ufaulu wa chini anaoupata mwanafunzi huyo, utamwezesha mwalimu kugundua tatizo na kulitatua;
- (iv) kuandaa vigezo vyta kutumia wakati wa kuwapanga wanafunzi katika madaraja kwa kuzingatia viwango vyta ufaulu ili kuchagua wanafunzi wanaotakiwa kuendelea na madarasa ya juu na wanafunzi wanaotakiwa kurudia darasa kutokana na kushindwa kumudu umahiri na stadi za ngazi husika.
- (v) Kubaini wanafunzi wenye umahiri wa kuweza kujieleza na kujenga hoja na kujiamini, hivyo kuandaa rasilimali watu wenye ujuzi na weledi wa kuweza kuchangia katika ujenzi wa uchumi wa nchi yao.
- (vi) kuwapa wanafunzi changamoto ya kujifunza na kujenga tabia ya kujisomea zaidi kwani kwa kufanya upimaji

wanafunzi watakuwa na ufahamu kuwa baada ya kufundishwa na kujifunza watapimwa.

- (vii) kuwezesha shule husika kujua ufanisi wake katika kutekeleza mtaala wa elimu katika ngazi husika ikilinganishwa na shule nyingine.
- (viii) kuwashauri viongozi wa elimu kuhusu ubora au mapungufu ya mitaala inayotumika.

## **2.3 Aina za Upimaji**

Zipo aina nne za upimaji ambazo ni upimaji wa awali, upimaji endelevu, upimaji tatuji/gunduzi na upimaji tamati. Aidha, aina hizi zote za upimaji zina malengo katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi.

### **2.3.1 Upimaji wa Awali (Placement Assessment)**

Upimaji wa awali hufanyika kabla mtoto hajaanza shule au mara tu anapoanza shule ili kubaini uwezo wake na ikiwa ana tatizo lolote linaloweza kukwamisha ujifunzaji wake. Vilevile, upimaji huu humsaidia mwalimu kufuatilia historia ya mtoto na familia yake, changamoto na vipaji alivyonavyo. Taarifa za upimaji huu zinaweza kutokana na kuwahoji wazazi wa mtoto au mwanafunzi na kumchunguza kwa kufuatilia jinsi anavyojoieleza.

### **2.3.2 Upimaji Endelevu (Formative Assessment)**

Upimaji endelevu hufanyika wakati mafunzo yanaendelea ambapo mwalimu hutumia zana mbalimbali kama vile; mazoezi ya darasani, upimaji wa kila wiki, kila mwezi na mwisho wa muhula. Upimaji huu humsaidia mwalimu, mzazi na mwanafunzi kujua maendeleo ya mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji endelevu hufanyika ili kuona kama mwanafunzi anamudu stadi alizofundishwa kabla ya kufanya upimaji tamati. Upimaji endelevu hutumika:

- (i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi.

- (ii) Kuboresha mbinu na njia za ufundishaji ili kumsaidia mwanafunzi.
- (iii) Kutoa mrejesho kwa wakati.
- (iv) Kubaini wanafunzi wanaohitaji mafunzo ya ziada.
- (v) Kuandaa taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi.

### **2.3.3 Upimaji Tatuzi/Gunduzi (Diagnostic Assessment)**

Upimaji tatuzi/gunduzi hulenga kutafuta kwa undani sababu zinazomfanya mwanafunzi kutoshiriki katika vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, hufanyika wakati mwalimu anapoolekeza wanafunzi kufanya kitendo fulani na kubaini kuwa hawashiriki ipasavyo katika ufundishaji na ujifunzaji au hawaelewi kinachoendelea. Upimaji huu hutumika;

- (i) kuandaa mafunzo mahususi kwa wanafunzi.
- (ii) kupata taarifa ya mahitaji ya wanafunzi katika kujifunza.

### **2.3.4 Upimaji Tamati (Summative Assessment)**

Aina hii ya upimaji hufanyika kwa kuunganisha taarifa zilizopatikana katika upimaji wa awali, endelevu na tatuzi ili kupata taarifa sahihi ya mabadiliko ya mtoto katika nyanja zote za kiakili, kimwenendo na kistadi. Upimaji huu hufanyika mwishoni mwa mafunzo au muhula ili kutathmini kiwango cha mafanikio kwa ajili ya kuendelea na mafunzo katika ngazi inayofuata. Upimaji tamati hutumika:

- (i) kupima maarifa na stadi alizopata mwanafunzi mwishoni mwa mafunzo.
- (ii) kubaini mambo yanayotakiwa kupewa kipaumbele katika kumfundisha mwanafunzi.
- (iii) kutathmini ubora wa mafunzo au mtaala.

### **3.0 UTHABITI NA KUAMINIKA KWA JARIBIO**

Ili kupima umahiri wa wanafunzi kwa usahihi, mwalimu anatakiwa kuzingatia uthabiti na kiwango cha ubora wa maswali ya jaribio.

#### **3.1 Uthabiti wa Jaribio (Reliability of a Test)**

Uthabiti wa jaribio hutokana na usahihi wa maswali yaliyoulizwa na ambayo yanaweza kutumika kupima wanafunzi katika maeneo tofauti na kutoa matokeo yanayofanana (consistency).

##### **3.1.1 Mambo yanayoathiri Uthabiti wa Jaribio**

- (a) Urefu wa jaribio: Idadi ya maswali yanayoulizwa kwenye jaribio ina athari kubwa kwenye uthabiti wa mtihani au jaribio husika. Maswali yanapokuwa mengi yanatoa nafasi kwa mwanafunzi kupimwa katika maeneo mengi aliyofundishwa hivyo kuweza kubaini kiasi cha maarifa na stadi alizopata. Aidha, jaribio likiwa na maswali machache sana matokeo yatakayopatikana hayawezi kutoa tathimini sahihi kuhusu uwezo wa wanafunzi wanaopimwa. Hata hivyo ni vema urefu wa jaribio uzingatie umri na ngazi ya Elimu ya mwanafunzi.
- (b) Kiwango cha ugumu wa maswali: Endapo maswali yaliyoulizwa kwenye jaribio ni magumu au rahisi sana kwa wanafunzi, kuna uwezekano wa kupata matokeo yanayotoa tafsiri isiyo sahihi kuhusu uwezo wa wanafunzi husika. Hivyo jaribio bora linatakiwa kuwa na maswali ya aina zote (rahisi na magumu) yanayoendana na ngazi ya wanafunzi na kupima maarifa na stadi walizofundishwa.
- (c) Maelekezo ya jaribio: Maelekezo ya wazi na fasaha yanaongeza uthabiti wa jaribio. Aidha, maelekezo yenye utata yasioeleweka bayana kwa wanafunzi yanasaababisha mwanafunzi kushindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kukosa majibu yanayotarajiwa kutoka kwa wanafunzi husika.

- (d) Mazingira: Mazingira ya ufanyikaji wa jaribio yanatakiwa kuwa rafiki na ya usawa kwa wanafunzi wote. Kuwe na mpangilio mzuri wa samani na kuhakikisha zinapatikana kwa wanafunzi wote. Aidha, kuhakikisha uwepo wa mwanga wa kutosha. Mazingira ya ufanyikaji wa jaribio yasipokuwa ya usawa baadhi ya wanafunzi wanaweza kuathirika kwa kushindwa kufanya jaribio vizuri au wengine kunufaika.

### **3.2 Kuaminika kwa Jaribio (Validity of a Test)**

Kuaminika kwa jaribio huonekana kama maswali yanapima nyanja ambazo zinapaswa kupimwa. Maswali yanatakiwa kutathimini umahiri wa wanafunzi waliouputa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji (Learning outcomes). Hivyo yanatakiwa kubeba uzito unaostahili kwa kila umahiri unaopimwa.

#### **3.2.1 Mambo Yanayoathiri Kuaminika kwa Jaribio**

Mambo yafuatayo huathiri kuaminika kwa jaribio:

- (a) Urefu wa jaribio: Iwapo jaribio litakuwa fupi sana au refu sana (maswali machache/mengi sana) kiasi cha matokeo ya jaribio hilo kushindwa kutoa tafsiri sahihi kuhusu uwezo wa wanafunzi waliopimwa, jaribio hilo haliwezi kuaminika kama kipimo sahihi cha stadi mbalimbali walizojifunza wanafunzi.
- (b) Maelekezo yasioeleweka: Iwapo maelekezo ya jaribio kuhusu namna ya kujibu maswali hayaeleweki vizuri kwa wanafunzi kuaminika kwa jaribio hilo kama kipimo sahihi kunapungua. Hivyo, wanafunzi wanaweza kujibu maswali kinyume na matarajio ya walimu kisha kutoa matokeo na taswira tofauti ya uwezo wao.
- (c) Ugumu wa misamiati: Misamiati katika sentensi ni maneno yanayomsaidia mtahiniwa au mwanafunzi kuelewa nini anatakiwa kufanya. Misamiati migumu inaweza kusababisha

mtahiniwa au mwanafunzi ashindwe kuelewa matakwa ya swali kwa ufasaha.

- (d) Muundo wa sentensi: Sentensi ndefu iliyoundwa kwa maneno mengi inaweza kumfanya mwanafunzi ashindwe kuelewa maana au matakwa ya swali kwa urahisi. Matokeo ya upimaji yanaweza yasitoe tathmini sahihi kuhusu uwezo wa wanafunzi kutokana na wanafunzi hao kutumia muda mwingu kujaribu kuelewa maana iliyokusudiwa katika sentensi. Aidha, mwanafunzi anaweza kushindwa kupata majibu ya maswali aliyoulizwa au kushindwa kumaliza kujibu maswali yote ya upimaji.
- (e) Maswali yasiyoendana na hatua waliyofikia wanafunzi: Iwapo maswali yaliyotungwa hayaendani na kiwango cha umahiri waliofundishwa wanafunzi na kufanya jaribio kuwa rahisi sana au gumu sana kwao, matokeo ya jaribio hilo hayawezi kuaminika.
- (f) Maswali kuandaliwa bila kuzingatia kanuni na taratibu za uandaaji wa jaribio: Maswali ya jaribio yanayotoa au kumsaidia mwanafunzi /mtahiniwa kupata majibu kwa urahisi (clues) pasipo kufikiri husababisha matokeo ya jaribio hilo yasiaminike.
- (g) Sentensi zenyе utata (ambiguity): Sentensi tata katika jaribio husababisha tafsiri tofauti au kumchanganya mwanafunzi, hivyo matokeo ya jaribio husika kushindwa kuwatofautisha wanafunzi husika.
- (h) Uwepo wa maswali yasioendana na malengo ya upimaji yaliyokusudiwa: Iwapo watunzi wa maswali ya jaribio watatunga maswali zenyе kiwango cha juu (Higher order Thinking Skills) wakati umahiri na maudhui yanayopimwa yanahitaji kiwango cha chini cha kufikiri (Lower Order Thinking Skills) kama vile, maarifa kuhusu mtiririko wa hatua za kufanya jambo

fulani kunaweza kuathiri kuaminika kwa jaribio. Hivyo, kutunga maswali ya ngazi ya juu kwa umahiri au maudhui yanayotakiwa kupimwa kwa maswali ya ngazi ya chini kunaweza kusababisha malengo yaliokusudiwa yasifikasiwe na kufanya jaribio lisiaminike.

- (i) *M pangilio mbaya wa maswali:* Maswali katika jaribio hutakiwa kuzingatia ugumu wa maswali husika ambapo maswali rahisi hutakiwa kuanza yakifuatiwa na maswali magumu. Iwapo maswali magumu yataanza katika jaribio yatawafanya wanafunzi kutumia muda mwangi katika maswali hayo na kushindwa kujibu au kuyafikia maswali mengine ambayo wangeweza kuyajibu kwa urahisi na hivyo kukata tamaa. Hivyo, mpangilio mbaya wa maswali huathiri ubora wa jaribio kwa kuwa matokeo yake hayawezi kutoa tathmini halisi kuhusu uwezo wa wanafunzi.
- (j) *M pangilio maalumu wa majibu:* Kwa maswali *yanayohitaji majibu mafupi* kama vile maswali ya kuchagua jibu sahihi, kweli au si kweli na kuoanisha, mpangilio wa majibu unatakiwa usitoe nafasi ya mwanafunzi kubuni jibu sahihi. Endapo mpangilio wa majibu hautakuwa wa kiwango kinachotakiwa na mwanafunzi kugundua uwepo wa mpangilio maalum (Pattern) mfano T, T, F, F, T, T au A , B, C, D; anaweza kubuni majibu ya maswali yanayofuata kwa urahisi. Jambo hili humfanya mpimaji kupata matokeo yasiyotarajiwa kutoka kwa wanafunzi.
- (k) *Mazingira yasiyofaa ya kufanya upimaji:* Mazingira yenyе kelele, mwanga hafifu, vitisho, vifaa/zana na kemikali zenye kuhatarisha usalama yanaweza kuathiri utulivu na umakini wa wanafunzi na hatimaye kusababisha matokeo ya jaribio husika kutokuaminika.
- (l) *Uendeshaji na usahihishaji wa jaribio:* Hatua za uendeshaji na usahihishaji wa jaribio

zilizoandaliwa na mwalimu zinaweza kuathiri kuaminika kwa jaribio. Kwa mfano, muda usiotosheleza wa kufanya jaribio, wanafunzi kusaidiana kinyume na utaratibu, udanganyifu na usahihishaji usio makini hutoa tafsiri tofauti ya uwezo wa wanafunzi.

- (m) *Aina ya kundi la wanafunzi wanaopimwa:* Mambo kama vile umri wa wanafunzi, jinsi, uwezo, historia ya kitaaluma na utamaduni wa jamii wanamoishi yanaweza kuathiri matokeo ya jaribio. Hivyo, aina ya kundi linalopimwa ni kigezo muhimu cha kuzingatia wakati wa kuandaa maswali ya jaribio ili kupata matokeo yaliyokusudiwa.

### 3.3 Hatua za Kutunga Maswali Bora ya Upimaji

Ili kutunga maswali yenye ubora, mwalimu anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- (a) *Kubainisha malengo ya jaribio:* Katika hatua hii, mwalimu anapaswa kubainisha malengo ya jaribio. Malengo yanaweza kuwa kupima maendeleo ya mwanafunzi katikati ya ufundishaji na ujifunzaji au kupima uwezo wa mwanafunzi wa kumudu stadi katika kipindi chote cha mafunzo kwa ngazi husika. Hivyo, mwalimu kabla ya kutunga maswali na kuyaweka katika karatasi ya upimaji, anapaswa kuzingatia malengo ya jaribio lake.
- (b) *Kuandaa jedwali la upimaji:* Katika hatua hii, mwalimu anapaswa kuandaa jedwali la upimaji. Jedwali hilo litamwezesha kuandaa maswali kutoka katika umahiri mbalimbali kutokana na uzito wake katika muhtasari wa somo husika. Vilevile, jedwali hilo litamuongoza mwalimu kusambaza maswali katika nyanja mbalimbali za utambuzi kama vile; kukumbuka, kuelewa, kuchambua, kutumia, kutathmini na kuunda.

- (c) *Kuchagua aina sahihi ya maswali:* Mwalimu anatakiwa kufanya maamuzi juu ya aina ya maswali yanayotakiwa kuwepo katika karatasi ya upimaji. Hatua hii huzingatia ngazi ya wanafunzi, muda utakaotumika kufanya upimaji na umahiri utakaopimwa.

### 3.4 Upimaji Unaozingatia Umahiri

Upimaji unaozingatia umahiri unalenga kubaini stadi na umahiri wa wanafunzi katika viwango vya utendaji. Upimaji wa aina hii hufanyika ili kubainisha uwezo wa mwanafunzi katika kutenda jambo fulani. Huu ni upimaji ambao unapima stadi za wanafunzi pamoja na umahiri kwa kulinganisha na vigezo vya utendaji wao vilivyowekwa kama vile: hafifu, wastani, vizuri na vizuri sana.

Upimaji unaozingatia umahiri ni njia ya upimaji iliyoboreshwa ambayo ni tofauti na upimaji unaozingatia maarifa ya wanafunzi pekee. Njia hii ina mchango mkubwa katika kuboresha elimu na hivyo kuzalisha watendaji bora katika maeneo mbalimbali na kwa jamii kwa ujumla.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapima umahiri wa wanafunzi ili kukidhi matakwa ya maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na Sera ya Elimu inayoelekeza Taifa kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Katika maendeleo hayo, jamii itahitaji watu wenge stadi za juu za utendaji kazi ambazo zinaweza kufikiwa kuititia upimaji unaozingatia umahiri wa wanafunzi.

Upimaji unaozingatia umahiri unajikita katika kutathmini uwezo wa wanafunzi kutenda jambo kulingana na maarifa waliyonayo, kufikiri kwa kina, kuchambua mambo, kujenga hoja, kutathmini na kutoa ushauri wenge kujenga zaidi au kuboresha. Hivyo, upimaji unaozingatia umahiri unapima stadi katika nyanja za juu za kufikiri. Lengo ni kuwaandaa watu wanaoweza kufikiri kwa usahihi, kuchambua na kuelezea masuala mbalimbali, kutatua matatizo katika mazingira na kutoa maoni na mapendekezo kwa kuzingatia ushahidi. Jedwali Na. 1 linaonesha sampuli ya maswali yanayopima umahiri na yale

yanayopima uwezo wa mwanafunzi kukariri maarifa na stadi mbalimbali.

**Jedwali Na 1: Sampuli ya Maswali yanayopima Umahiri  
Ikilinganishwa na Maswali Yanayopima  
Uwezo wa Kukariri**

<b>Na.</b>	<b>Maswali Yanayopima Umahiri</b>	<b>Maswali Yanayopima Uwezo wa Kukumbuka</b>
1.	<p>“Sisi ni wanafunzi hodari wa somo la Kiswahili.” Kauli hii imeundwa katika nafsi ipi kati ya hizi zifuatazo?</p> <p>A Nafsi ya kwanza umoja B Nafsi ya pili umoja C Nafsi ya tatu umoja D Nafsi ya kwanza wingi E Nafsi ya pili wingi.</p>	<p>Ni neno lipi kati ya yafuatayo linawakilisha nafsi ya kwanza wingi?</p> <p>A Mimi B Yeye C Wao D Sisi E Ninyi</p>
2.	<p>Mwaka 1985 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamua kung’atuka madarakani na kumwachia Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. Kitendo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kung’atuka kinamaanisha nini?</p> <p>A Kuaga wafanyakazi B Kukaimisha madaraka C Kustaafu kazi D Kujiuzulu madaraka E Kupumzika kazi kidogo.</p>	<p>Kisawe cha neno kung’atuka ni kipi kati ya maneno yafuatayo:</p> <p>A Kuaga wafanyakazi B Kukaimisha madaraka C Kustaafu kazi D Kujiuzulu madaraka E Kupumzika kazi kidogo.</p>
3.	<p>The opposite of the underlined word in the sentence, “They <u>arrived</u> from Tanga at 8.00 am” is _____.</p> <p>A left B took-off C departed</p>	<p>What is the opposite of the word arrived?</p> <p>A left B took-off C departed D flew E gone</p>

<b>Na.</b>	<b>Maswali Umahiri</b>	<b>Yanayopima</b>	<b>Maswali Uwezo wa Kukumbuka</b>
	D flew E gone		
4.	<p>Wakulima wengi nchini Tanzania hupeleka mazao sokoni kuza. Ni njia zipi kuu za usafirishaji zinazotumika?</p> <p>A Barabara na reli B Anga na barabara C Maji na anga D Reli na anga E Maji na barabara</p>	<p>Njia kuu za usafirishaji nchini ni</p> <p>A Barabara na reli B Anga na barabara C Maji na anga D Reli na anga E Maji na barabara</p>	
5.	<p>Katika anga kuna mkusanyiko wa hewa mbalimbali kwa viwango tofauti. Je, ni aina gani ya hewa hupatikana kwa wingi?</p> <p>A Naitrojeni B Oksijeni C Kabonindayoksaidi D Haidrojeni E Kabonimonoksaidi</p>	<p>Hewa inayopatikana kwa wingi angani ni_____.</p> <p>A Naitrojeni B Oksijeni C Kabonindayoksaidi D Haidrojeni E Kabonimonoksaidi</p>	
6.	<p>Kazimoto alichagua wanafunzi watano ili waandike kipeuo cha pili cha jumla ya namba witiri zilizopo kuanzia 1 hadi 11. Je, lipi ni jibu sahihi katika majibu yafuatayo?</p> <p>A 3              B 5 C 4              D 2 E 6</p>	<p>Kipeuo cha pili cha 36 ni</p> <p>A 3              B 5 C 4              D 2 E 6</p>	
7.	Tafuta zao la uzito wa kilogramu 0.9 za unga na kilogramu 3.12 za mchele.	$0.9 \times 3.12?$ <p>A 2.889              B 2.789 C 28.89              D 29.89</p>	

<b>Na.</b>	<b>Maswali Yanayopima Umahiri</b>	<b>Maswali Yanayopima Uwezo wa Kukumbuka</b>
	A 2.889      B 2.789 C 28.89      D 29.89 E 4.11	E 4.11
8.	Katika gesi zifuatazo, ipi unaweza kuitumia kuzima kitu kinachowaka? A Oksijeni. B Nitrojeni. C Kabonimonoksaidi. D Hyadrojeni. E Kabonidayoksaidi.	Gesi inayotumika kuzima moto ni _____. A Oksijeni. B Nitrojeni. C Kabonimonoksaidi. D Hyadrojeni. E Kabonidayoksaidi.
9.	Umepewa kazi ya kutafuta densiti ya maji. Je utatoa jibu lako katika kizio gani? A Kg/m <sup>3</sup> B J/sm <sup>3</sup> C N/m <sup>3</sup> D Kg/sm <sup>3</sup> E m/sm <sup>3</sup>	Kizio cha densiti ni? A Kg/m <sup>3</sup> B J/sm <sup>3</sup> C N/m <sup>3</sup> D Kg/sm <sup>3</sup> E m/sm <sup>3</sup>
10.	Jina la Tanzania lilianza kutumika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Je, ni mwaka gani jina hilo lilianza kutumika? A 1962      B 1967      C 1964 D 1992      E 1961	Tanganyika na Zanzibar ziliungana mwaka _____. A 1962      B 1967      C 1964 D 1992      E 1961
11.	Haki za binadamu nchini Tanzania zinalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, ni mwaka gani haki za binadamu ziliingizwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? A 1965      B 1964      C 1992 D 1961      E 1984.	Sheria za haki za binadamu zilianza kutumika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka _____. A 1965      B 1964      C 1992 D 1961      E 1984.
12.	Wahitimu wa Darasa la Saba waliosoma somo la	Taja manufaa ya elimu ya uraia?

Na.	Maswali Yanayopima Umahiri	Maswali Yanayopima Uwezo wa Kukumbuka
	Uraia na Maadili, wanawezaje kunufaisha jamii zao kwa elimu hiyo waliyoipata?	

#### 4.0 TAKSONOMIA YA BLOOM

Taksonomia ya Bloom ni mwongozo muhimu wa kuunda orodha kamili ya malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha Taxonomia hiyo inatambua na kuainisha matokeo yote yanayowezekana ya elimu. Kutokana na Bloom, kuna nyanja kuu tatu za kujifunza; Nyanja ya Utambuzi (Cognitive Domain), Nyanja ya Utendaji/Ujuzi (Psychomotor Domain) na Nyanja ya Mwelekeo (Affective Domain).

##### 4.1 Nyanja ya Utambuzi (Cognitive Domain)

Nyanja ya Utambuzi inahusu maendeleo ya kitaaluma ya mwanafunzi. Nyanja hii imegawanyika katika hatua sita; Kukumbuka (Remembering), Kuelewa (Understanding), Kutumia (Applying), Kuchambua (Analysing), Kutathmini (Evaluating) na Kuunda (Creating).

##### 4.2 Nyanja ya Mwelekeo (Affective Domain)

Nyanja ya Mwelekeo huhusisha madhumuni ambayo husitiza hisia na maono kama vile mwelekeo, kuridhia na mbinu za kujirekebisha. Nyanja hii imegawanyika katika viwango vitano kama ifuatavyo; Upokeaji (Receiving), Mwitikio (Responding), Uthamani (Valuing), Mpango (Organising) na Mwenendo (Characterisation).

##### 4.3 Nyanja ya Stadi (Psychomotor Domain)

Nyanja hii ya Stadi huhusisha malengo yote yanayosisitiza matendo maalumu ya stadi mbalimbali kama vile uandikaji (mwandiko), kufanya vitendo kama vile kufanya majaribio, upigaji chapa, uogeleaji na uendeshaji wa mashine mbalimbali. Nyanja hii imegawanyika katika ngazi za kutoka

chini kwenda juu. Inahusisha stadi ambazo ni; Uchambuzi, Kuiga, Tathmini na Mazoezi.

Mwongozo huu umejikita zaidi kwenye Nyanja ya Utambuzi. Nyanja hii hutoa njia ya kupanga stadi za kufikiri katika ngazi sita, kutoka ngazi ya chini zaidi hadi ngazi ya juu ya kufikiri. Aidha, Taksonomia ya Bloom iliyoboreshwa mwaka 1990, imebainisha maboresho kadhaa yalifanywa katika ngazi (Kategoria) za utambuzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 2.

### **Jedwali Na. 2: Taksonomia Iliyoboreshwa na ya Zamani**

<b>Taksonomia ya Zamani</b>	<b>Taksonomia Iliyoboreshwa</b>
Tathmini (Evaluation)	Kuunda (Creating)
Uundaji (Synthesis)	Kutathmini (Evaluating)
Uchambuzi (Analysis)	Kuchambua (Analysing)
Matumizi (Application)	Kutumia (Applying)
Ufahamu (Comprehension)	Kuelewa (Understanding)
Maarifa (Knowledge)	Kukumbuka (Remembering)

Maboresho yaliyofanywa katika Taksonomia ya Bloom ni katika majina ya ngazi sita kuu kutoka nomino hadi vitenzi, kwani kufikiria ni mchakato wa vitendo, vitenzi vilioneekana kuwa sahihi zaidi.

#### **4.4 Umuhimu wa Taksonomia ya Bloom**

Taksonomia ya Bloom ina umuhimu kama ifuatavyo:

- Inasaidia walimu kubuni kazi za utendaji, utunzi wa maswali na kutoa maoni juu ya kazi za wanafunzi.
- Inasaidia walimu katika kuandika malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.
- Inasaidia waandaaji wa mitaala na walimu katika kuhakikisha kuwa nyanja zote za wanafunzi wanaosoma zinazingatiwa katika mchakato wa kujifunza.

- (d) Inatoa mwongozo kwa walimu kujikita katika kuandaa maswali yanayopima ngazi ya juu ya kufikiri (Higher Order Thinking).

Vitenzi vinavyotumika katika kila ngazi ya Bloom na sampuli ya maswali ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.3.

**Jedwali Na. 3: Vitenzi na Sampuli ya Maswali yanayotumika katika Ngazi mbalimbali za Taksonomia ya Bloom**

Na.	Ngazi ya Bloom	Uwezo Unaopimwa	Vitenzi Vinavyotumika	Sampuli ya Swali
1.	Ngazi ya I: Kukumbuka	Uwezo wa mwanafunzi kukumbuka mambo aliyojifunza.	orodhesha, onesha, taja, oanisha, simulia, chagua na tambua.	<p>(a) Taja mwaka ambao Tanganyika na Zanzibar ziliungana.</p> <p>(b) Bendera ya taifa la Tanzania ina rangi ngapi?</p> <p>(c) Nini maana ya Uraia na Maadili?</p> <p>(d) Bahari ya Hindi ipo upande gani katika ramani ya Tanzania?</p>
2.	Ngazi ya II: Kuelewa	Uwezo wa mwanafunzi katika kuelewa jambo au tukio.	elezea kwa maneno yako, simulia, fupisha, panga katika makundi, oanisha, linganisha, tofautisha, tafsiri, onesha, badili, kadiria, toa mfano, tetea na eleza.	<p>(a) Tofautisha kati ya Uraia na Maadili.</p> <p>(b) Eleza ujumbe uliokusudiwa katika kifungu cha habari ulichosoma.</p> <p>(c) Fupisha kifungu cha habari ulichosoma kwa kutumia maneno hamsini.</p> <p>(d) Eleza kwa kutumia maneno mengine, jinsi unavyoweza kuzuia mmomonyoko wa</p>

<b>Na.</b>	<b>Ngazi ya Bloom</b>	<b>Uwezo Unaopimwa</b>	<b>Vitenzi Vinavyotumika</b>	<b>Sampuli ya Swali</b>
				udongo.
3.	Ngazi ya III: Kutumia	Uwezo wa mwanafunzi katika kutatua matatizo katika mazingira mengine kwa kutumia maarifa, mbinu, kanuni aliyojifunza.	tumia, unda, chagua, fumbua, kokotoa, badili, rekebisha, onesha na tatua.	<p>(a) Onesha aina mbili za wajibu ambao umewahi kutekeleza kama raia wa Tanzania.</p> <p>(b) Badili 75% kuwa katika sehemu rahisi.</p> <p>(c) Kutokana na taarifa uliyopewa onesha namna utakavyoishauri jamii yako kuvala nguo zenyestaha kwa miktadha mbalimbali.</p> <p>(d) Kokotoa eneo la pembetatu yenye kitako cha sm 3 na egemeo la sm 5</p> <p>(e) Matendo yapi mawili yanaonesha usawa wa kijinsia?</p>
4.	Ngazi ya IV: Kuchambua	Kipengele hiki kinahusu uchambuzi wa dhana, tukio au maarifa fulani. Katika uchambuzi, upimaji unalenga kuona uwezo wa mwanafunzi katika kuchunguza	Chambua, panga katika makundi, linganisha, pima, tofautisha, gawa, rahisisha na fupisha.	<p>(a) Tofautisha kati ya tabia ya unafiki na ya uwazi.</p> <p>(b) Chambua maana ya msamati katika kifungu cha habari uliyosoma.</p> <p>(c) Bainisha sifa tano za tabia ya usafi.</p> <p>(d) Changanya sentensi ifuatayo: Juma na Roza wanakwenda shulen kusoma.</p> <p>(e) Panga maneno yafuatayo kuwa</p>

<b>Na.</b>	<b>Ngazi ya Bloom</b>	<b>Uwezo Unaopimwa</b>	<b>Vitenzi Vinavyotumika</b>	<b>Sampuli ya Swalii</b>
		na kutaja uhusiano wa mambo, kwa mfano, uwezo wa mwanafunzi katika kuchambua sentensi mbalimbali. .		sentensi kamili: nyumbani, Amina, usiku, jana, alikuja.
5.	Ngazi ya V: Kutathmini	Uwezo wa mwanafunzi katika kutetea hoja au wazo kwa kuthibitisha kwa kutumia vigezo vilivyowekwa .	chagua, hitimisha, amua, tetea, tathmini, pima, thibitisha, pendeleza, kadiria, kosoa, kataa, fananisha na hoji.	(a) Je, unakubaliana na hoja kwamba utandawazi ni janga kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania? (b) Ni nini msimamo wako kuhusu hoja kwamba “Utandawazi ni janga kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania?” (c) Ni kipaji kipi kizuri kati ya uimbaji wa nyimbo za dini na uchezaji wa mpira wa miguu? (d) Ipi kati ya njia zifuatazo ni sahihi katika kuhifadhi mazingira: kupanda miti na kulima kandokando ya mito? (e) Andika faida tatu za kuvalaa mavazi yenye staha.

<b>Na.</b>	<b>Ngazi ya Bloom</b>	<b>Uwezo Unaopimwa</b>	<b>Vitenzi Vinavyotumika</b>	<b>Sampuli ya Swali</b>
				(f) Je, unakubaliana kwamba Tanzania inafaidika kuwa mwanachama wa Jumuia ya Umoja wa Mataifa?
6.	Ngazi ya VI: Kuunda	Uwezo wa mwanafunzi katika kuunganisha taarifa/habari katika njia tofauti kwa kuunganisha vipengele mbalimbali katika muundo mpya au suluhisho jipya.	unganisha, unda, kadiria, tatua, badili, punguza, panga, buni, sanifu, panga upya, fupisha, thibitisha, weka pamoja na boresha.	(a) Andika insha ya maneno 50 kuhusu faida za utandawazi. (b) Ni kwa namna gani unaweza kuboresha mazingira ya shule yako? (c) Pang'a sentensi zifuatazo katika mtiririko weny'e kuleta mantiki. (d) Ni kwa namna gani unaweza kuboresha mahudhurio ya wanafunzi katika shule za kutwa? (e) Weka pamoja mikakati ya kuzuia UVIKO-19 nchini Tanzania. (f) Kwa kutumia picha zifuatazo ; andika taarifa kuhusu matukio yaliyobainishwa katika picha.

## **5.0 HATUA ZA KUANDAA MTIHANI/JARIBIO**

Mwalimu anapoamua kuandaa mtihani/jaribio anapaswa kufuata hatua mbalimbali zitakazomsaidia kufanya mtihani/jaribio lake kuwa na viwango vinavyotakiwa ili kupata matokeo halisi. Wakati wa kuandaa jaribio mwalimu anapaswa kufanya yafuatayo:

- (a) Kutayarisha jedwali la utahini;
- (b) Kuandaa maswali;
- (c) Kurekebisha maswali;
- (d) Kuendesha upimaji ipasavyo;
- (e) Kusahihisha jaribio kwa kufuata mwongozo wa usahihishaji uliosanifiwa; na
- (f) Kurekodi alama alizopata kila mwanafunzi.

### **5.1 Utayarishaji wa Jedwali la Utahini**

Kabla mwalimu hajaanza kutunga maswali anapaswa kutayarisha Jedwali la Utahini. Jedwali la Utahini ni chati inayooonesha umahiri utakaopimwa, idadi ya maswali katika kila umahiri, nyanja ya utambuzi pamoja na stadi inayopimwa na asilimia ya uzito kwa kila umahiri unaopimwa.

### **5.2 Malengo ya Kuandaa Jedwali la Utahini**

Malengo ya kuandaa Jedwali la Utahini ni kama yafuatavyo:

- (a) Kuhakikisha kuwa kuna uwiano kati ya maudhui yaliyofundishwa na yale yanayopimwa. Mtihani/jaribio ni lazima lioneshe uwiano uliopo kati ya maudhui na ujuzi kulingana na umuhimu wake wakati wa ufundishaji. Mathalani, maudhui yaliyopewa kipaumbele (yaliyofundishwa kwa muda mwangi zaidi) hayana budi kupewa uzito zaidi katika mtihani/jaribio.
- (b) Kuhakikisha kuwa mtihani au jaribio linaloandaliwa linajumuisha yale yaliyofundishwa pekee.
- (c) Kuonesha uhusiano kati ya ufundishaji na upimaji.
- (d) Kupata mwongozo wa kutengeneza maswali ya upimaji.

(e) Kupata uzito wa kila umahiri uliofundishwa katika utunzi wa mtihani au jaribio.

(f) Kuhakikisha sampuli wakilishi ya maswali yaliyotungwa kwa kila maudhui inaendana na uzito wa kila umahiri.

### **5.3 Mambo Muhimu ya Kuzingatia Wakati wa Kuandaa Jedwali la Kutahini**

Yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa wakati wa kuandaa jedwali la utahini:

(a) Kubainisha malengo ya somo. Wakati au kabla ya kuandaa jedwali la utahini, mwalimu au mpimaji anapaswa kubainisha malengo ya somo.

(b) Kubaini vipengele vya umahiri vilivyokwishafundishwa darasani.

(c) Kubainisha kiasi cha muda (idadi ya vipindi/saa) uliotumika kufundisha vipengele hivyo vya umahiri.

(d) Kubaini idadi ya vipindi kama vilivyoainishwa kwenye muhtasari.

(e) Kubaini idadi ya maswali katika kila umahiri.

(f) Kubaini jumla ya idadi ya maswali ya upimaji kwa kuzingatia fomati ya upimaji.

(g) Kubainisha ngazi za nyanja ya utambuzi (Cognitive Levels).

### **5.4 Hatua za Kuandaa Jedwali la Kutahini**

Jedwali la kutahini linaundwa na safu nne ambapo safu ya kwanza kushoto huwekwa maudhui (umahiri mahususi utakaopimwa), safu inayofuata huwekwa nyanja inayopimwa (utambuzi) pamoja na stadi zake ambazo ni; Kukumbuka, Kuelewa, Kutumia, Kuchambua, Kutathmini na Kuunda. Pia, safu inayofuata huwekwa jumla ya maswali kwa kila mada na safu ya mwisho huwekwa asilimia kwa kila mada. Aidha, jumla ya maswali kwa kila ngazi na asilimia huandikwa kwenye mstari wa chini wa jedwali. Hatua za kufuata wakati wa kuandaa Jedwali la Kutahini ni kama ifuatavyo:

- (i) Orodhesha malengo/ umahiri mahususi wa somo.
- (ii) Bainisha umahiri mahususi uliokwishafundishwa.
- (iii) Bainisha muda uliotumika kufundisha kila umahiri (idadi ya vipindi/ saa zilizotumika katika kila umahiri).
- (iv) Kokotoa asilimia ya muda uliotumika kufundisha umahiri mahususi.
- (v) Kokotoa idadi ya maswali kwa kila umahiri kulingana na muda uliotumika kufundisha umahiri husika.

**Mfano:**

- (a) Chukulia umahiri uliokwishafundishwa na muda uliotumika kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Umahiri Uliofundishwa na Muda Uliotumika katika Ufundishaji Somo la Kiswahili**

Na.	Umahiri Mahususi	Muda Uliotumika Kufundisha (Idadi ya Vipindi)
1.	Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.	7
2.	Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.	6
3.	Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali.	7
<b>Jumla</b>		<b>20</b>

- (b) Tumia kanuni ifuatayo kukokotoa asilimia (%) ya uzito wa kila umahiri katika mtihani:

% ya Uzito wa Umahiri

$$= \frac{\text{Muda wa Kufundisha Umahiri}}{\text{Jumlaya mudawa kufundisha mahiri zote}} \times 100$$

Kwa mfano, umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo* katika miktadha *mbalimbali* ulifundishwa kwa vipindi 7 na jumla ya vipindi vilivyotumika kufundisha vipengele vyote vya umahiri ni vipindi 20. Hivyo, ili kupata asilimia ya uzito wa umahiri huo katika mtihani, ukokotozi utafanyika kama ifuatavyo:

$$\text{Uzito wa umahiri} = \frac{7}{20} \times 100 = 35\%$$

Asilimia ya uzito wa umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo* katika miktadha *mbalimbali* ni asilimia 35. Kanuni hiyo itatumika kukokotoa katika vipengele vyote vya umahiri na kupata data kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 5.

#### **Jedwali Na. 5: Uzito wa kila Umahiri**

<b>Na.</b>	<b>Umahiri Mahususi</b>	<b>Idadi ya Vipindi</b>	<b>% ya Muda Uliotumika katika Umahiri</b>
1.	Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha <i>mbalimbali</i> .	7	35
2.	Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha <i>mbalimbali</i> .	6	30
3.	Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha <i>mbalimbali</i> .	7	35
<b>Jumla</b>		<b>20</b>	<b>100</b>

(c) Chukulia, kwa mfano, jumla ya maswali katika mtihani ni 40, tumia kanuni ifuatayo kukokotoa idadi ya maswali katika kila umahiri:

$$\text{Jumla ya maswali katika umahiri} \\ = \frac{\% \text{ ya uzito wa Umahiri}}{100} \times \text{Jumlanya maswali}$$

Kwa mfano, umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo* katika miktadha mbalimbali una uzito wa asilimia 35 na jumla ya maswali katika mtihani ni 40. Hivyo, ili kupata jumla ya maswali ya umahiri huo yanayotakiwa katika mtihani kokotoa kama ifuatavyo;

$$\text{Idadi ya maswali katika umahiri} = \frac{35}{100} \times 40 = 14$$

Hivyo, umahiri wa *kuanzisha na kuendeleza mazungumzo* utakuwa na maswali 14 kati ya 40 ya jaribio zima. Kanuni hiyo itatumika kukokotoa katika vipengele vyote vya umahiri na kupata data kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6.

#### **Jedwali Na. 6: Idadi ya Maswali katika Kila Umahiri**

Na	Umahiri Mahususi	Idadi ya Vipindi	% ya muda Uliotumika katika Umahiri	Idadi ya Maswali katika Umahiri
1.	Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.	7	35	14
2.	Kutumia msamati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.	6	30	12
3	Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali.	7	35	14
<b>Jumla</b>		<b>20</b>	<b>100</b>	<b>40</b>

- (a) Amua aina ya maswali unayotaka kutumia katika upimaji kama vile; maswali ya kuchagua, kweli/si kweli, kuoanisha, kujaza au kutoa majibu mafupi kwa

kuzingatia umahiri uliokwisha fundisha kutoka kwenye muhtasari.

- (b) Panga maswali kwenye kila umahiri kwa kuzingatia malengo au umahiri uliokusudiwa kupimwa kama linavyoonekana katika Jedwali Na. 7.

#### **Jedwali Na. 7: Mfano wa Jedwali la Utahini katika Somo la Kiswahili**

Na.	<b>Umahiri Mahususi</b>	<b>Nyanja za Utambuzi Zitakazopimwa</b>						<b>Idadi ya Maswali</b>	<b>Asilimia ya Uzito kwa kila Umahiri</b>
		Kukumbuka	Kuelewa	Kutumia	Kuchambua	Kutathmini	Kuunda		
1.	Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali.	2	2	2	3	2	3	14	35
2.	Kutumia msamati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali.	2	2	2	2	2	2	12	30
3.	Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali.	2	3	3	2	2	2	14	35
<b>Idadi ya Maswali kwa kila Nyanja</b>		<b>6</b>	<b>7</b>	<b>7</b>	<b>7</b>	<b>6</b>	<b>7</b>	<b>40</b>	
<b>Asilimia ya Uzito wa Maswali kwa kila Nyanja</b>		<b>15</b>	<b>17.5</b>	<b>17.5</b>	<b>17.5</b>	<b>15</b>	<b>17.5</b>		<b>100</b>

#### **6.0 UTUNGAJI WA MASWALI YA MTIHANI/JARIBIO**

Utungaji wa maswali ya upimaji au mitihani ni mchakato wa kisayansi na wa kisanaa. Mchakato wa kisayansi unahusisha uzingatiaji wa kanuni, sheria na miongozo katika utunzi wa maswali

ya mtihani au jaribio bora. Mchakato wa kisanaa unahusisha mwonekano wa jaribio kwa maana ya mpangilio na ubora wa maswali, muundo wa sentensi, matumizi sahihi ya misamiati, mpangilio mzuri wa michoro au vifungu vya habari. Uwepo wa jaribio bora unategemea sana uthabiti wa mchakato wa utungaji na urekebishaji wa maswali. Mwalimu anapoandaa maswali ya Mtihani anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- (a) Kupima matokeo yote yanayohitajika.
- (b) Kutambua malengo ya somo na maudhui yake.
- (c) Kupima malengo yote kwa uwiano wa umuhimu wa malengo husika na idadi ya maswali katika mtihani.
- (d) Kuhakikisha maelekezo kuhusu mtihani yanayotolewa yanajitosheleza na hayana utata.
- (e) Msamiati na vitenzi vinavyotumika katika maswali yote vinaeleweka.
- (f) Lugha inayotumika ni sanifu na inaendana na kanuni za kisarufi za lugha inayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo husika.
- (g) Kila aina ya swali inajibainisha katika sehemu, kama vile sehemu A maswali ya kuchagua jibu moja sahihi, sehemu B maswali ya kuoanisha, sehemu C maswali ya Kweli Si kweli na sehemu D maswali ya majibu mafupi. Hivyo, aina za maswali zisichanganywe katika sehemu moja.
- (h) Mwongozo wa usahihishaji unaandalawa kwa kuzingatia matakwa ya swali husika na mgawanyo wa alama unaoneshwa bayana.

## 6.1 Aina za Maswali

Aina za maswali yanayotumika mara kwa mara katika upimaji ni kama ifuatavyo:

- (a) Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi
- (b) Maswali ya Kuoanisha
- (c) Maswali ya Kweli/Si Kweli

- (d) Maswali ya Majibu Mafupi
- (e) Maswali ya Insha

#### **6.1.1 Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi**

Maswali ya kuchagua jibu sahihi ni maswali ambayo mwanafunzi hujibu kwa kuchagua jibu moja sahihi kutoka kwenye orodha ya machaguo aliyopewa. Maswali haya huundwa na mzizi na chaguzi ambapo mzizi hutambulisha swali au tatizo na chaguzi ni majibu ambayo huwa na jibu sahihi moja na vipotoshi au vichachawizi. Wataalamu wa upimaji wanaeleza kuwa, maswali haya ndiyo maswali mazuri kuliko aina nyingine ya maswali kwa kuwa yana uwezo wa kupima nyanja zote, kuanzia Kukumbuka hadi Kuunda, yanaweza kupima eneo kubwa la maudhui kwa wakati mmoja na husahihishwa kwa urahisi. Aina za maswali ya kuchagua ni kama ifuatavyo:

- (a) Maswali ya kuchagua yaliyoandaliwa kwa kuuliza swali.
  - (i) Wanawake na wanaume wana wajibu na majukumu tofauti katika jamii. Ni dhana gani inafanua wajibu na majukumu hayo?
    - A Jinsia\*
    - B Wanaume
    - C Jinsi
    - D Wanawake
    - E Familia



\*Herufi A ni jibu sahihi  
Herufi B, C, D na E ni vipotoshi.

- (ii) Unapaswa kufanya nini unapokuwa katika eneo linapopandishwa au kushushwa Bendera ya Taifa?

- A Ondoka haraka sana.
- B Tembea kwa madaha.
- C Simama kwa heshima.\*
- D Endelea na shughuli zako.
- E Simamisha magari.

\* Herufi C ni jibu sahihi  
Herufi A, B, D na E ni vipotoshi.

(b) Sentensi isiyokamilika.

Hii ni aina ya maswali ya kuchagua jibu sahihi ambapo swali huulizwa kwa kutoa sentensi ambayo haijakamilika. Kwa mfano:

- (i) Njia inayoweza kuchochea maendeleo ya nchi kwa haraka katika sekta mbalimbali ni \_\_\_\_\_.

- A Kushiriki katika michezo
- B Kufanya kazi kwa bidii\*
- C Kuomba misaada nje ya nchi
- D Kudumisha mila na desturi zetu
- E Kuongeza idadi ya walimu shulenii

\* Herufi B ni jibu sahihi  
Herufi A, C, D na E ni vipotoshi.

- (ii) Mtu anayeishi sehemu zenyeye baridi kali anatakiwa kula kwa wingi chakula chenye \_\_\_\_\_.

- A protini
- B wanga
- C vitamini
- D madini
- E mafuta\*

\*Herufi E ni jibu sahihi

Herufi A, B, C na D ni vipotoshi.

- (c) Maswali yaliyoandaliwa kwa sentensi iliyokamilika. Maswali ya mtindo huu huwa na sentensi iliyokamilika katika kuwasilisha mzizi wa swali. Kwa mfano:

Ni miaka mingapi ya uhuru wa Tanzania mpaka kufikia mwaka 2020 ?

- A Miaka 49  
B Miaka 59\*  
C Miaka 69  
D Miaka 29  
E Miaka 85

\*Herufi B ni jibu sahihi.

Herufi A, C, D & E ni vipotoshi.

#### **6.1.1.1 Manufaa ya Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi**

Maswali ya kuchagua jibu sahihi yana manufaa yafuatavyo:

- (a) Hupima vipengele vyote katika nyanja ya utambuzi.  
(b) Hupima umahiri na ujuzi mwingi kwa wakati mmoja.  
(c) Hutoa matokeo yenyе uhakika.  
(d) Yakitungwa vizuri, huweza kuhusisha maswali yanayohusu utatuzi wa matatizo.  
(e) Hupunguza uwezekano wa mwanafunzi kubuni majibu kutokana na uwepo wa chaguzi zinazoshabihiana.  
(f) Huweza kusahihishwa kwa muda mfupi.  
(g) Huweza kusahihishwa kwa mshine (kompyuta).

#### **6.1.1.2 Udhafu wa Maswali ya Kuchagua**

- (a) Ni magumu sana kuyaanda.  
(b) Hayawezi kupima uwezo wa kujenga hoja.  
(c) Hayawezi kupima uwezo wa kujieleza.

### 6.1.1.3 Misingi ya Utungaji wa Maswali ya Kuchagua Jibu

(a) Shina la swali liwe linajitosheleza lenyewe.

#### Mfano wa swali zuri

Mtu asiyepokea ushauri wa wengine huishia kuharibikiwa katika maisha. Ni methali ipi itafaa kufikisha ujumbe huu?

- A Asiyekuwepo machoni na moyoni hayupo.
- B Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.\*
- C Asiye na mengi ana machache.
- D Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.
- E Asiyeuliza hana ajifunzalo.



\* Herufi B ni jibu sahihi

Herufi A, C, D & E ni vipotoshi

*Shina la swali linajitosheleza kwani matakwa ya swali yako wazi.*

#### Mfano wa swali hafifu

Mtu asiyepokea ushauri wa wengine huishia kuharibikiwa katika maisha. Ni sawasawa na

- A Asiyekuwepo machoni na moyoni hayupo.
- B Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.\*
- C Asiye na mengi ana machache.
- D Asiyeangalia huishia ningalijua.
- E Asiyeuliza hana ajifunzalo.



\*Herufi B ni jibu sahihi

Herufi A, C, D & E ni vipotoshi.


*Matakwa ya swali hayako wazi hivyo mwanafunzi atashindwa kuelewa swali linataka nini.*

- (b) Shina la swali liwe linabeba sehemu kubwa ya swali.

**Mfano wa swali zuri**

Historia ya ukombozi wa Tanzania inajengwa na mabadiliko ya chama cha TAA kuwa TANU mwaka 1954. Lengo la mabadiliko hayo lilikuwa ni

- 
- A Kuwaunganisha watu wote katika kudai uhuru\*
  - B Kuwa chama cha kisiasa kwa ajili ya wafanyakazi tu
  - C Kuwaunganisha watu wote kupigana vita vya ukombozi
  - D Kuongeza nguvu ya wafanyakazi katika kudai uhuru
  - E Kuwa chama cha kutetea ustawi wa wakulima



\*Herufi A ni jibu sahihi.

Herufi B, C, D na E ni vipotoshi

*Shina la swali linafafanua kuwa TAA ni chama cha wafanyakazi kilichotumika katika harakati za ukombozi ambacho baadaye kilibadilishwa na kuwa TANU hali inayomsaidia mwanafunzi kuelewa vizuri mzizi wa swali.*

### **Mfano wa swali hafifu**

Kwa nini TAA ilibadilishwa kuwa TANU?

- A Kuwaunganisha watu wote katika kudai uhuru\*
- B Kuwa chama cha kisiasa kwa ajili ya wafanyakazi tu.
- C Kuwaunganisha watu wote kupigana vita vyaa ukombozi.
- D Kuunganisha vyama vyote vyaa siasa katika harakati za ukombozi.
- E Kuwa chama cha kutetea ustawi wa wakulima.

\*Herufi A ni jibu sahihi.

Herufi B, C, D na E ni vipotoshi

*Shina la swali haliko wazi kwani haijulikani TAA ni kitu gani hali inayoweza kumtatiza mwanafunzi.*

- (c) Tumia vikanushi pale tu unapoona kuna ulazima/umuhimu wa kufanya hivyo.

### **Mfano**

Zifuatazo ni faida za urejelezaji wa taka,  
**isipokuwa**

- A watu kupata ajira.
- B utunzaji wa mazingira.
- C kupunguza ongezeko la joto duniani.\*
- D ongezeko la rutuba katika udongo.
- E kupunguza kuenea kwa magonjwa.

\*Herufi C ni jibu sahihi.

Herufi A, B, D na E ni vipotoshi

*Katika swali hili umuhimu wa neno **isipokuwa** ni kutaka kupima kama mwanafunzi anaweza kubainisha faida za urejelezaji wa taka.*

- (d) Shina na chaguzi lazima viwe na upatanisho wa kisarufi.

**Mfano wa swali zuri**

Upendo is joyful. The word “joyful” means \_\_\_\_\_.

- A happy\*
- B sad
- C angry
- D awkward
- E wonderful

\*Herufi A ni jibu sahihi.

Herufi B, C, D & E ni vipotoshi

*Katika swali hili kuna upatanisho wa kisarufi kati ya shina na chaguzi.*

**Mfano wa swali hafifu**

Upendo is joyful. The word “joyful” is \_\_\_\_\_.

- A happy\*
- B sad
- C angry
- D awkward
- E wonderful

\*Herufi A ni jibu sahihi.

Herufi B, C, D & E ni vipotoshi

*Katika swali hili hakuna upatanisho wa kisarufi kati ya shina na chaguzi. Aidha kutumia neno “is” kunafanya swali kutokuwa wazi hivyo kuwa na uwezekano wa kuwepo utata.*

- (e) Kila swali liwe na jibu moja tu ambalo ni sahihi zaidi.

**Mfano wa swali zuri**

Ipi kati ya sehemu zifuatazo ni sehemu rahisi ya 45%?

- A  $\frac{5}{20}$       B  $\frac{8}{20}$       C  $\frac{9}{20}^*$       D  $\frac{12}{20}$       E  $\frac{15}{20}$

Jibu pekee sahihi katika swali hili ni C, yaani  $\frac{9}{20}$

**Mfano wa swali hafifu**

Ipi kati ya sehemu zifuatazo inawakilisha 45%?

- A  $\frac{5}{20}$       B  $\frac{8}{20}$       C  $\frac{9}{20}^*$       D  $\frac{12}{20}$       E  $\frac{18}{40}$

\* Herufi C na E ni majibu sahihi  
Herufi A, B & D ni vipotoshi

*Mtunzi wa swali hili anaonesha kuwa jibu sahihi ni chaguo C  $\frac{9}{20}$  pekee ingawa chaguo E  $\frac{18}{40}$  nalo ni*

*jibu sahihi. Swali kama hili haliwezi kupima uwezo halisi wa wanafunzi kwani mwanafunzi atakayechagua C na atakayechagua E kama jibu sahihi wote watakuwa wamepata kwa sababu  $\frac{18}{40}$*

*ikirahisishwa unapata  $\frac{9}{20}$  na zote ukizibadili kuwa asilimia unapata asilimia 45.*

- (f) Vipotoshi vyote lazima viwe na ushawishi wa kuchaguliwa.

**Mfano wa swali zuri**

Wingi wa sentensi “Nimeamua kusoma kwa bidii” ni upi kati ya sentensi zifuatazo?

- A Wameamua kusoma kwa bidii.
- B Umeamua kusoma kwa bidii.
- C Mmeamua kusoma kwa bidii.
- D Tumeamua kusoma kwa bidii.\*
- E Ameamua kusoma kwa bidi.

\*Herufi D ni jibu sahihi

Herufi A, B, C & E ni vipotoshi

*Katika swalii hili machaguo yote yanaweza kumvutia mwanafunzi, hivyo inatakiwa kabla mwanafunzi hajaweza kubaini jibu sahihi lazima awe na uelewa wa kutosha kuhusu nafsi za uwingu na umoja zinavyotumika.*

### **Mfano wa swali hafifu**

Wingi wa sentensi “Nimeamua kusoma kwa bidii” ni upi kati ya sentensi zifuatazo?

- A Wameamua kusoma
- B Umeamua kusoma
- C Mmeamua kusoma
- D Tumeamua kusoma kwa bidii\*
- E Ameamua kusoma

\*Herufi D ni jibu sahihi

Herufi A, B, C na E ni vipotoshi

*Katika swalii hili mwanafunzi ni rahisi kubaini jibu sahihi kwa kuwa linajitofautisha wazi na chaguzi nyiningine.*

- (g) Hakikisha kuwa hakuna uhusiano wa maneno kati ya shina na chaguzi.

### **Mfano wa swali zuri**

Maeneo yafuatayo ya kihistoria yanapatikana  
**Tanzania isipokuwa**

- A Rusinga.\*
- B Oldvai Gorge.
- C Engaruka.
- D Kondoa Irangi.
- E Kaole.

\*Herufi A ni jibu sahihi

Herufi B, C, D na E ni vipotoshi

*Maneno yaliotumika kwenye shina hayana  
uhusiano wa moja kwa moja na chaguzi.*

### **Mfano wa swali hafifu**

Maeneo yafuatayo ya kihistoria yanapatikana  
**Tanzania isipokuwa**

- A Rusinga\*
- B Oldvai Gorge Arusha
- C Engaruka Arusha
- D Kondoa Irangi Dodoma
- E Kaole Bagamoyo

\*Herufi A ni jibu sahihi

Herufi B, C, D na E ni vipotoshi


*Chaguzi B, C, D na E yanaonesha sehemu  
yalipo maeneo ya kihistoria yaliyobainishwa  
wakati chaguzi **A Rusinga** hajulikani  
linapatikana sehemu gani katika Tanzania hali  
inayomrahisishia mwanafunzi kubaini jibu  
sahihi.*

- (h) Chaguzi zote ziwe na urefu unaokaribia  
kufanana.

### **Mfano wa swali zuri**

Historia ya ukombozi wa Tanzania inajengwa na mabadiliko ya chama cha TAA kuwa TANU mwaka 1954. Lengo la mabadiliko hayo lilikuwa ni \_\_\_\_\_

- A Kuwaunganisha watu wote katika kudai uhuru\*
- B Kuwa chama cha kisiasa kwa ajili ya wafanyakazi tu
- C Kuwaunganisha watu kupigana vita vya ukombozi
- D Kuongeza nguvu ya wafanyakazi katika kudai uhuru
- E Kuwa chama cha kutetea ustawi wa wakulima



\*Herufi A ni jibu sahihi.

Herufi B, C, D na E ni vipotoshi

*Katika swali hili chaguzi zinakaribiana kwa urefu.*

### **Mfano wa swali hafifu**

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anatambulika kuwa ni shujaa wa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Ni nini kinachomfanya atambulike hivyo?

- A Alikuwa mstari wa mbele kупinga vikali aina zote za ubaguzi wa rangi na kidini.\*
- B Ni mwanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- C Alihusika kuanzisha mfumo wa vyama vingi.
- D Aliwapenda sana waafrika kuliko wazungu.
- E Alishiriki katika Mapinduzi ya Zanzibar.



\*Herufi A ni jibu sahihi.  
Herufi B, C, D na E ni vipotoshi


*Katika swali hili, jibu sahihi ni refu zaidi kuliko chaguzi zingine hali inayoweza kumsaidia mwanafunzi kubaini jibu sahihi kwa urahisi.*

- (i) Majibu sahihi ya maswali yatawanywe katika herufi zote za chaguzi na katika idadi iliyo sawa ili kuzuia mwanafunzi kubashiri majibu. Mfano ikiwa kuna vipengele 10 vya maswali ya kuchagua, hakikisha majibu ya maswali hayo yana mchanganyiko wa herufi za majibu sahihi.
- (j) Maneno “hakuna jibu lililo sahihi”; “majibu yote ni sahihi” yasitumike.

#### **Mfano wa swali zuri**

*When children visited one of the National Parks, they were given an instrument that helped them see animals which were very far. Which instrument do you think they were given?*

- A Microscope    B Periscope    C Telescope\*
- D Eye glasses    E Camera



\*Herufi C ni jibu sahihi.  
Herufi A, B,D na E ni vipotoshi

#### **Mfano wa swali hafifu**

*When children visited one of the National Parks, they were given an instrument that helped them see animals which were very far. Which instrument do you think they were given?*

- |               |                      |                          |
|---------------|----------------------|--------------------------|
| A Microscope  | B Periscope          | C Camera                 |
| D Eye glasses | E No correct answer* | <input type="checkbox"/> |

\*Herufi E ni jibu sahihi.

Herufi A, B, C na D ni vipotoshi

*Uwepo wa neno “No correct answer” katika chaguzi kunapunguza wigo wa kumfikirisha mwanafunzi kwa kuwa anabakiwa na chaguzi nne badala ya tano.*

### 6.1.2 Maswali ya Kuoanisha

Maswali ya kuoanisha hupima umahiri wa mwanafunzi katika kutafuta uhusiano kati ya masuala au mambo mawili. Masuala haya huwa na mafungu mawili ambayo huwa katika safu mbili, safu ya mzizi (Safu/Orodha A) na majibu (Safu/Orodha B). Mambo yanayooneshwaa ni maneno, namba na picha kwa ajili ya kuoanisha. Kwa mfano, sentensi inaweza kuoanishwa na fasili, tarehe na matukio, aina ya vifaa/vitu na majina yao na methali kuoanishwa na majibu yake.

#### 6.1.2.1 Manufaa ya Maswali ya Kuoanisha

- (a) Hupima umahiri katika nyanja za Maarifa na Ufahamu.
- (b) Hupima vitu vinavyoshabihiana.
- (c) Ni rahisi kuyasahihisha.

#### 6.1.2.2 Udhaifu wa Maswali ya Kuoanisha

- (a) Hupima zaidi uwezo wa kukumbuka mambo.
- (b) Ni vigumu kutayarisha kutohana na ugumu wa kupata mambo yanayoshabihiana.

### **6.1.2.3 Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Kuoanisha**

Misingi ya utayarishaji wa maswali ya kuoanisha ni kama ifuatavyo:

- (a) Tumia mambo yanayoshabihiana katika zoezi moja la kuoanisha.
- (b) Toa maelekezo bayana yatakayomwongoza mwanafunzi kufanya zoezi la kuoanisha bila matatizo.
- (c) Zoezi moja la kuoanisha liwe katika ukurasa mmoja ili kuzuia usumbufu kwa upande wa wanafunzi kutafuta majibu. Hivyo, ni vema swali la kuoanisha likawa na vipengele vitano.
- (d) Weka orodha ya majibu katika mpangilio wa kimantiki, kwa mfano mpangilio wa kialfabeti (kwa kuanza na herufi A hadi E), au kutoka namba ndogo kwenda namba kubwa.
- (e) Ikiwa baadhi ya majibu yanaweza kutumika zaidi ya mara moja ielezwe kwenye maelekezo.
- (f) Maswali katika fungu au orodha A yawe na matakwa yanayojitosheleza kuliko majibu katika fungu au orodha B.
- (g) Majibu katika orodha B yanatakiwa kuwa mafupi ili kumfanya mwanafunzi asitumie muda mrefu kutafuta jibu.
- (h) Katika orodha B ya majibu sahihi yawepo majibu ya ziada mawili au matatu yasiyo sahihi. Majibu hayo yachanganywe na majibu sahihi ili iwe ngumu mwanafunzi kubuni.

**Mifano ya Maswali ya Kuoanisha ni kama ifuatavyo:**

**Mfano wa maswali mazuri**

- Oanisha matukio muhimu katika historia ya Tanzania yaliyoko katika **Fungu A** na miaka yalipotokea katika **Fungu B** kwa kuandika **herufi ya mwaka** mbele ya namba ya tukio katika karatasi ya kujibia.

<b>Na.</b>	<b>Fungu A</b>	<b>Majibu</b>	<b>Fungu B</b>
(i)	Uhuru wa Tanganyika	( )	A 1961 B 1962
(ii)	Mapinduzi ya Zanzibar	( )	C 1963
(iii)	Tanganyika kuwa Jamhuri	( )	D 1964 E 1967
(iv)	Sera ya Siasa ni Kilimo	( )	F 1971
(v)	Azimio la Arusha	( )	G 1972

**Majibu Sahihi**

<b>Orodha A</b>	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)
<b>Jibu</b>	A	D	B	G	E

Katika swali hili orodha **A** ina vipengele **5** na vyote vinabainisha matukio muhimu ya kihistoria na orodha **B** ina miaka inayohusiana na matukio husika hivyo

kufanya swali hili kuundwa na vipengele vinavyotokana na shina/mzizi mmoja (homogeneity).

2. Oanisha matumizi ya vifaa katika **Orodha A** na majina ya vifaa hivyo kutoka **Orodha B** kisha andika **herufi ya jibu sahihi** kwenye mabano uliyopewa.

<b>Orodha A</b>	<b>Majibu</b>	<b>Orodha B</b>
(i) Kifaa kinachotumika kupima mwendokasi wa upepo ulio katika mwendo.	( )	A Haigromita B Kipima mvua C Kipimajoto
(ii) Kifaa kinachotumika kupima msukumo wa hewa.	( )	D Baromita E Anemometa
(iii) Kifaa kinachotumika kupima kiwango cha unyevu au mvuke wa maji yaliyo ndani ya hewa katika anga.	( )	F Themomita G Nivometa
(iv) Kifaa kinachotumika kupima hali ya joto au baridi ya kitu au mahali.	( )	
(v) Kifaa kinachotumika kupima kiwango cha mvua.	( )	

#### **Majibu Sahihi**

<b>Orodha A</b>	1	2	3	4	5
<b>Jibu</b>	E	D	A	F	B

Katika zoezi hili, orodha **A** ina maswali **5** na yote yanabainisha matukio ya hali ya hewa

na orodha **B** vifaa vinavyotumika kupima matukio hayo hivyo kufanya swali hili kuwa na *homogeneity*.

### **Mfano wa swali hafifu**

Oanisha sentensi katika **Orodha A** na maneno kutoka **Orodha B** kisha andika **herufi ya jibu sahihi** kwenye mabano uliyopewa.

<b>Orodha A</b>	<b>Majibu</b>	<b>Orodha B</b>
(i) Mto mkubwa katika Tanzania.	( )	A Madagasca
(ii) Mji mkuu wa Zambia	( )	B Kenya, Uganda, Kongo, Rwanda na Sudan Kusini
(iii) Muasisi wa Taifa la Tanzania	( )	C Lusaka
(iv) Wanachama wa Afrika Mashariki	( )	D J.K.Nyerere
(v) Visiwa vinavyopatikana bahari ya Hindi	( )	E Malagarasi
		F Kitwe
		G Zambezi

### **Majibu Sahihi**

<b>Orodha A</b>	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)
<b>Jibu</b>	E	C	D	B	A

Katika swali hili orodha **A** ina sentensi za maswali **5** ambazo zinapima dhana tofauti (mito, visiwa, historia, pamoja na mahusiano ya nchi) na orodha **B** ni maneno yanayohusiana na sentensi hizo hivyo kufanya swali hili kuundwa na vipengele kutoka kwenye mashina/mizizi tofauti (lack homogeneity).

### **6.1.3 Maswali ya Kweli/Si kweli**

Katika maswali ya Kweli/Si kweli, mwanafunzi hupimwa uwezo wa kubaini iwapo sentensi, msemo au dhana aliyopewa ni ya kweli au siyo ya kweli. Maswali haya hujikita zaidi katika kupima uwezo wa kubainisha vitu vyta kweli na visivyo vyta kweli kwa kupima zaidi kukumbuka au kuelewa mambo, vitu au dhana fulani. Maswali haya ni rahisi kutunga na kusahihisha ingawa yana udhaifu ufuatao:

- (i) Ni rahisi mwanafunzi kubuni jibu kwa kuandika kweli au si kweli pasipo kuelewa dhana husika.
- (ii) Ni rahisi kufanya udanganyifu ikiwa usimamizi ni dhaifu.
- (iii) Hupima ngazi za chini za kufikiri.

#### **Mifano ya Maswali ya Kweli/Si kweli ni kama ifuatavyo:**

1. Maelekezo: Soma kila sentensi kati ya hizi zifuatazo. Kama sentensi hiyo ni kweli zungushia herufi **K** na kama si kweli zungushia herufi **S**.

<b>K</b>	<b>S</b>	Usanisinuru ni mchakato wa majani ya kijani kibichi kutengeneza chakula cha mmea.
<b>K</b>	<b>S</b>	Nchi ya inapatikana mwa Afrika. Tanzania magharibi

2. Maelekezo: Soma kila sentensi kati ya hizi zifuatazo. Kama jibu ni ndio zungushia herufi **N** na kama jibu ni hapana zungushia herufi **H**.

<b>N</b>	<b>H</b>	Je 50% ya namba 38 ni zaidi ya 18?
<b>N</b>	<b>H</b>	Je, Mbuga ya Taifa ya Wanyama ya Serengeti inapatikana Kenya?

3. Maelekezo: Soma kila sentensi kati ya hizi zifuatazo: Kama sentensi hiyo ni ya Ukweli zungushia herufi **K** na kama ni Maoni basi zungushia herufi **M**.

<b>K</b>	<b>M</b>	Nchi zingine hazina budi kuwa na katiba kama ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
<b>K</b>	<b>M</b>	Tanganyika ilipata uhuru wake mwaka 1961.

4. Maelekezo: Katika kipengele cha (i)-(v), andika **Sahihi** ikiwa sentensi ni sahihi na **Si sahihi** ikiwa sentensi sio sahihi.

(i) Katika mfumo wa mmeng'enywa wa chakula, virutubisho hufyonzwa kwenye utumbo mpana. Si sahihi

- (ii) Kiwavi ni hatua ya ukuaji wa kipepeo inayosababisha uharibifu mkubwa kwenye mazao. Sahihi
- (iii) Upinde wa mvua ni matokeo ya mwanga kusharabiwa. Si sahihi
- (iv) Hofu ya kifo ndiyo madhara pekee anayopata mtu anayeishi na VVU. Si sahihi
- (v) Kuzima moto kwa kutumia blanketi hakupunguza nguvu ya moto unaowaka.  
Sahihi

#### **6.1.3.1 Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Kweli/Si kweli**

Misingi ya utayarishaji wa maswali ya Kweli au Si kweli ni kama ifuatavyo:

- (a) Usitumie sentensi zenyе maelezo ya jumla kwani swali halitakuwa na mantiki.

##### **Mfano Hafifu:**

Mbu hueneza ugonjwa wa malaria.

*Katika swali hili haijabainishwa ni aina gani ya mbu anaeneza ugonjwa wa malaria kwani si mbu wote wanaoeneza ugonjwa huo.*

**Mfano Sahihi:** Mbu *anopheles* hueneza ugonjwa wa malaria.

*Swali limebainishwa aina ya mbu anayeeneza ugonjwa wa malaria.*

- (b) Usiulize mambo ambayo hayana tija kwa mwanafunzi.

**Mfano Hafifu:** Afisa Mtendaji wa Kata ya Kunjamguu anaitwa Jumamosi Mwezi.

*Jina la kata na Afisa Mtendaji havimsaidii mwanafunzi katika maisha yake ya kila siku. Hivyo, swali hili halina tija yoyote katika kukuza au kubaini umahiri wa mwanafunzi kuhusu ngazi za uongozi na majukumu kwa kila ngazi.*

**Mfano Sahihi:** Kiongozi anayemwakilisha Mkurugenzi wa Wilaya katika kata huitwa Mtendaji wa Kata.

*Swali hili linapima uelewa wa mwanafunzi kuhusu ngazi za uongozi na majukumu yao.*

- (c) Usitumie sentensi kanushi bila sababu ya msingi.

**Mfano Hafifu:** Hakuna chakula ambacho **si** muhimu kwa mwili wa binadamu.

*Kinachopimwa katika swali hili ni umuhimu wa chakula katika mwili wa binadamu hivyo hakukuwa na ulazima wa kutumia si muhimu katika swali.*

**Mfano Sahihi:** Vyakula vyenye protini ni muhimu kwa mwili wa binadamu.

*Swali linapima iwapo mwanafunzi anatambua kama protini ni muhimu katika mwili wa binadamu. Aidha, linabainisha bayana aina ya chakula.*

- (d) Epuka sentensi ndefu zinazoweza kumchanganya mwanafunzi.

**Mfano Hafifu:** Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyetokea Mkoa wa Pwani, kijiji cha Msoga anaitwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

*Katika swali hili sentensi ni ndefu kiasi kwamba mwanafunzi anaweza asielewe swali linamaanisha nini.*

**Mfano Sahihi:** Rais wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaitwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

*Katika swali hili sentensi ni fupi na inaeleweka kwa urahisi.*

- (e) Usihusishe jambo zaidi ya moja katika hoja au sentensi moja.

**Mfano Hafifu:** Popo ni ndege kwasababu anaruka na ni mnyama kwasababu mwili wake umefunikwa na nywele.

*Swali lina hoja ya popo kuwa ndege, kuwa na uwezo wa kuruka, kuwa mnyama na mwili wake kufunikwa na nywele kwa wakati mmoja.*

**Mfano Sahihi:** Popo ni mnyama.

*Swali lina hoja moja tu ya ‘Popo ni mnyama’.*

- (f) Kama swali linahusu maoni, basi onesha chanzo cha maoni hayo.

**Mfano Hafifu:** Ubepari ni unyama.

*Swali linaonesha kuwa ni maoni.*

**Mfano Sahihi:** Kwa mujibu wa Baba wa Taifa Mwl. J. K. Nyerere, ubepari ni unyama.

*Swali linaonesha kuwa dhana ya ubepari kuwa unyama ni maoni/mtizamo wa Mwl. J. K. Nyerere.*

- (g) Urefu wa maswali ya kweli na yale ambayo si kweli yalingane.

**Mifano ya maswali hafifu ni kama ifuatayo:**

- (i) Ngorongoro, Serengeti na Manyara ni mbuga maarufu za wanyama nchini Tanzania. Kweli
- (ii) Utunzaji wa misitu ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi nchini Tanzaia inayosaidia usafirishaji na ukuaji wa viwanda nchini Tanzania. Si Kweli
- (iii) Anga na maji ndiyo njia kuu za usafirishaji zinazotumiwa na wakulima kupeleka mazao yao sokoni nchini Tanzania. Si Kweli

*Maswali katika mfano wa (ii) na (iii) ambayo jibu lake ni **Si kweli** ni marefu zaidi ukilinganisha na swali (i) ambalo jibu lake ni **Kweli**. Hivyo maswali yote aina hii yakitungwa kwa mfumo huu itakuwa rahisi kwa mwanafunzi kuweza kubaini jibu sahihi pasipo kufikiri kwa kina kwani atajua kuwa maswali yenye sentensi zenye maneno mengi jibu lake litakuwa ni **Si kweli** na zenye maneno machache jibu lake ni **Kweli**.*

- (h) Ikiwezekana, idadi ya maswali ya kweli na yale ambayo si kweli ilingane.
- (i) Maswali yenyе majibu sahihi yasiwe na mpangilio bainifu unaoweza kumfanya mwanafunzi aweze kubaini jibu sahihi pasipo kufikiri kwa kina.
- (j) Maneno kolezi katika maswali yasitumike kama vile; kamwe, mara kwa mara, mara nyingi, mara zote, zote, vyote, chote n.k.

#### **6.1.4 Maswali ya Majibu Mafupi**

Maswali ya majibu mafupi ni maswali ambayo mwanafunzi hutakiwa kutoa jibu sahihi kwa ufupi. Maswali mafupi huweza kupima uwanja mpana wa maarifa aliyoyapata mwanafunzi katika:

- (a) Ufahamu wa istilahi mbalimbali Mfano, kifaa kinachotumika kupima kasi ya upemo kinaitwa?
- (b) Ufahamu wa mambo/matukio mbalimbali. Mfano, Chama cha TANU na ASP viliungana mwaka gani?
- (c) Ufahamu wa kutafsiri taarifa fulani. Mfano kizio cha nyuzi za sentigredi 100 kinamaanisha nini katika jotoridi la maji?
- (d) Uwezo wa kukokotoa/kuchambua.

##### **6.1.4.1 Makundi ya Maswali ya Majibu Mafupi**

Katika ngazi ya Elimu Msingi aina ya maswali ya majibu mafupi yanayotumika zaidi katika kundi hili ni:

- (a) Maswali ya majibu mafupi.
- (b) Maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi.
- (c) Sentensi zilizochanganywa (Jumbled sentences).

##### **Mifano ya maswali yenyе kuhitaji majibu mafupi**

- (i) Nini tofauti kati ya mjasiriamali mtumishi na mjasiriamali mfanyabiashara?

**Jibu:** Mjasiriamali mtumishi ni mwajiriwa ambapo mjasiriamali mfanyabiashara anabuni na kufanya biashara.

(ii) Watu hujifunza kwa kushirikiana na kubadilishana maarifa na watu wengine katika jamii. Eleza faida mbili za kushirikiana katika kujifunza.

**Jibu:** (a) Hujenga tabia ya umoja na maelewano.

(b) Hujenga tabia ya uvumilivu.

(iii) Kwa nini wanyama wanahitaji gesi ya oksijeni?

**Jibu:** Wanyama wanahitaji gesi ya oksijeni kwa ajili ya resipiresheni ambayo matokeo yake huzalisha nishati.

### **Mifano ya maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi**

(i) Idadi ya wanafunzi waliohitimu Darasa la Saba mwaka 2018 katika kata yetu ilikuwa 600. Kati ya hao,  $7\frac{1}{2}\%$  hawakufaulu mtihani. Je, ni sehemu gani ya wahitimu walifaulu mtihani?

$$\text{Kazi: } 7\frac{1}{2}\% \text{ hawakufaulu} = \frac{7.5}{100} \times 600 = 45$$

$$\text{Kwa hiyo, waliofaulu} = 600 - 45 = 555$$

$$\text{Sehemu ya wanafunzi waliofaulu mtihani ni } \frac{555}{600}$$

$$= \frac{37}{40}$$

$$\text{Jibu: } \frac{37}{40}$$

- (ii) Chunguza Kielelezo kifuatacho kinachohusu mabadiliko ya kiumbo ya maji kisha jibu swalilinalofuata:



Katika kila herufi A mpaka D, bainisha mchakato unaosababisha mabadiliko ya hali moja kwenda nyingine kama mshale unavyoelekeza.

A \_\_\_\_\_

B \_\_\_\_\_

C \_\_\_\_\_

D \_\_\_\_\_

**Jibu:**

A ni kuyeyuka
B ni kuvukiza
C ni kuganda
D ni kupoa

- (iii) Sehemu ya mfumo wa chakula inayohusika katika kusharabu virutubisho kutoka kwenye chakula kilichomeng'enywa inaitwa

**Jibu:** Utumbo mwembamba

**Mfano wa sentensi zilizochanganywa (Jumbled sentences)**

1. Sentensi zifuatazo (i)-(v) zimeandikwa bila kuzingatia mtiririko sahihi. Zipange ili ziwe na

mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C, D.

- (i) Kila siku ninaamka asubuhi
- (ii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni
- (iii) Ninapiga mswaki na kuoga
- (iv) Mama ananipa chai na chapati
- (v) Ninakunywa chai na chapati.

**Jibu:** (i) A, (ii) E, (iii) B, (iv) C, (v) D

2. *This section has five mixed sentences (1-5). Arrange the sentences so as to make a meaningful composition by assigning them letters A-E besides the Arabic numbers in the answer sheet provided.*

- (i) *I hope that we shall meet during the December holidays at home.*
- (ii) *I wish you all the best in your examinations.*
- (iii) *Dear Kajala,*
- (iv) *I have heard that you will write your annual examinations in December, 2021.*
- (v) *Thank you for your letter.*

**Jibu:** (i) E, (ii) D, (iii) A, (iv) C, (v) B

#### **6.1.4.2 Manufaa ya Maswali ya Majibu Mafupi**

- (i) Ni rahisi kutunga kutoptana na ukweli kwamba yanapima ujuzi wa kiwango cha chini (simple learning outcomes) ukilinganisha na aina nyingine ya maswali.

- (ii) Si rahisi kubuni majibu kwa kuwa majibu yanatolewa na mwanafunzi mwenyewe badala ya kupewa machaguo ili aweze kuchagua jibu sahihi.
- (iii) Ni fasaha na maalumu kulingana na upana au urefu wa jibu linalotakiwa.
- (iv) Yana uwezo wa kupima mawanda mapana ya umahiri aliojifunza mwanafunzi.

#### **6.1.4.3 Udhifu wa Maswali ya Majibu Mafupi**

- (i) Yasipotungwa vizuri hayawezi kupima ujuzi wa kiwango cha juu. Mfano, utatuzi wa matatizo.
- (ii) Ni vigumu kusahihisha, hasa kama hayajatungwa vizuri.

#### **6.1.4.4 Misingi ya Utayarishaji wa Maswali ya Majibu Mafupi**

- (i) Uliza maswali ambayo majibu yake ni mafupi, wazi na hayana utata wowote.

#### **Mfano wa swali zuri**

Kutokana na habari uliyoisoma ni tabia gani mbaya alizokuwa nazo Kachiku? Taja mbili.

#### **Mfano wa swali hafifu**

Ni tabia gani za Kachiku ambazo hazivutii?

*Swali ni hafifu kwa sababu lina utata. Haileweke ni kachiku yupi anayezungumziwa katika swali ; Kachiku wa kwenye habari iliyosomwa au mwingine ye yote ambaye mwanafunzi atakuwa anamfahamu.*

- (ii) Usichukue sentensi moja kwa moja kutoka kwenye kitabu kama shina la swali kwa sababu linaweza kusababisha utata.

Mnyama anayekula nyama za wanyama wengine ni \_\_\_\_\_

- (iii) Mtindo wa swali la kawaida ni bora zaidi kuliko kutumia mtindo wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwasababu mtindo wa maswali ya sentensi isiyokamilika huweza kuwa na majibu mengi iwapo swali hilo halitatungwa vizuri.

**Mfano wa swali zuri**

*What is the collective name for the animals kept at home?*

**Mfano wa swali hafifu**

The animals kept at home are called \_\_\_\_\_.

*Swali ni hafifu kwasababu wapo wanyama wa aina nyingi wanaofugwa nyumbani hivyo swali linaweza kuwa na jibu sahihi zaidi ya moja.*

- (iv) Kama swali linahitaji kutoa vipimo fulani, onesha wazi kuwa ni vipimo gani vitatumika.

**Mfano wa swali zuri**

Peo tatu za shamba lenye umbo la mstatili ni A (-4, 1), B (-4,-2), na C (3,-2). Tumia grafu ya majira ya nukta kutafuta peo ya nne.

**Mfano wa swali hafifu**

Peo tatu za shamba lenye umbo la mstatili ni A (-4, 1), B (-4,-2) na C (3,-2). Tafuta peo ya nne.

*Swali ni hafifu kwasababu halioneshi njia gani mwanafunzi anatakiwa kutumia ili kupata jibu.*

- (v) Kama unatumia maswali ya kujaza nafasi, nafasi zisiwe nyingi katika swali moja.

- (vi) Nafasi inayatakiwa kujazwa iwe mwishoni au karibu na mwisho. Lengo ni kumpatia mwanafunzi fursa ya kutatua tatizo lililoelezwa katika sehemu ya mwanzo ya swali.

**Mfano wa swali zuri**

Mojawapo ya vyakula vya kuupa mwili nguvu ni

**Mfano wa swali hafifu**

Vyakula vya kuupa mwili nguvu ni \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_;

*Swali ni hafifu kwasababu linahitaji majibu matatu katika swali moja hali inayochochea kukariri majibu badala ya kufikiri kimantiki.*

#### **6.1.4.5 Aina za Maswali ya Majibu Mafupi (Objective Questions)**

Katika kipengele hiki maswali ya majibu mafupi yamechananuliwa kwa kuzingatia aina ya stadi inayopimwa na swali husika kama ifuatavyo:

- (i) Kumbukumbu ya kuchagua.

Mfano: Misingi ya Azimio la Arusha ni ipi?

- (ii) Kumbukumbu ya kutathmini.

Mfano: Benki ya biashara inatoa faida ya asilimia 4 kwa kiasi cha shilingi 200,000/= kwa mwezi. Faida kiasi gani itapatikana kwa akiba ya shilingi 1,500,000/= kwa mwaka?

- (iii) Ulinganifu wa vitu viwili katika msingi wa kitu kimoja.

Mfano: Linganisha faida za kutumia pasi ya umeme dhidi ya pasi ya mkaa.

- (iv) Ulinganifu wa vitu viwili kwa ujumla.  
Mfano: Linganisha shughuli za binadamu wakati wa zana za mawe za kale na zana za mawe za mwisho.
- (v) Kukubali au kupinga hoja.  
Mfano: Usiku na mchana ni matokeo ya dunia kujizungusha katika mhimili wake. Toa hoja mbili kuthibitisha ukweli huu.
- (vi) Sababu au madhara ya kufanya jambo fulani.  
Mfano: Kwa nini ni muhimu kuzingatia kanuni za maabara?
- (vii) Maelezo kuhusu matumizi au maana halisi ya tungo kutoka katika kifungu cha habari au sentensi.  
Mfano: Ukiwa kama mtaalamu wa lishe, eleza ni madhara gani mtu anaweza kuyapata endapo atashindwa kula mlo kamili?
- (viii) Uchambuzi.  
Mfano: Soma kwa makini orodha ya maneno iliyopo kwenye sanduku la maneno kisha yapange katika makundi yafuatayo: vivumishi, viwakilishi, vitenzi na vihisishi.
- (ix) Matumizi ya kanuni na misingi katika mazingira fulani.  
Mfano: Utatumia kanuni gani katika kukokotoa ujazo wa mche duara?
- (x) Kufupisha/kuandika kwa muhtasri kuhusu habari au hadithi.

Mfano: Fupisha habari ifuatayo kwa maneno yasiyozidi 50.

*Juhudi ni mtoto aliyelelewa na nyanya yake mzaa babake. Wazazi wake wote wawili walifariki kwa ajali ya gari Juhudi akiwa darasa la Pili. Juhudi alisoma hadi Chuo Kikuu ambapo alisomea fani ya Ualimu. Akiwa Chuo Kikuu, alifundishwa na wahadhiri mbalimbali katika masomo yake ya fani hiyo.*

*Baadaye Juhudi alihitimu masomo yake na kuajiriwa serikalini ambapo alikuwa mwalimu katika Shule ya Msingi Changanyikeni. Juhudi alikuwa ni mtu tegemeo sana katika shule hiyo kwa sababu alikuwa mahiri katika ufundishaji wa somo la Kiswahili. Wanafunzi walimpenda sana na walikuwa wanafaulu vizuri sana somo la Kiswahili.*

*Uongozi wa shule ulifurahia jitihada za Mwalimu Juhudi katika kazi yake. Kutokana na bidii katika kazi aliteuliwa kuwa mwalimu wa taaluma. Pamoja na majukumu ya ualimu wa taaluma bado aliendelea kufundisha somo la Kiswahili na waliendelea kufaulu vizuri somo hilo.*

- (xi) Uhusiano wa vitu.  
Mfano: Kazi za mwenge wa uhuru zinahusiana vipi na kazi za bendera ya Taifa.
- (xii) Kutumia mifano katika kuelezea kanuni za kisayansi, lugha n.k.  
Mfano: Kwa kutumia mifano miwili taja umuhimu wa alama za Taifa la Tanzania.

(xiii) Kueleza maana ya au kuelezea kitu.

Mfano: Eleza kwa ufupi madhara ya kutumia mkaa kwenye mazingira. Toa hoja mbili.

(xiv) Uwezo wa kutumia maarifa (interpretive short answer)

Mfano: Toa sababu mbili ni kwanini hakuna kazi inayofanyika kwa mtu anayesukuma ukuta?

(xv) Maswali yanayohitaji jibu likiwa katika mchoro

Mfano: Chora ramani ya Afrika Mashariki kuonesha maziwa makuu.

(xvi) Mswali ya kukokotoa.

Mfano: Kipenyo cha gurudumu moja la trekta ni mita  $1\frac{1}{2}$ . Tafuta mzingo wake.

## 7.0 MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

Mwongozo wa usahihishaji ni majibu yaliyoandaliwa kutohakikisha kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wanafunzi au watahiniwa wote waliojibu maswali, kwani watakuwa wanasherifikiwa kwa kufuata vigezo na alama zilizobainishwa.

Mwongozo wa usahihishaji unatakiwa kuandaliwa sambamba na utungaji wa maswali. Mtunzi anapaswa kubainisha jibu la swali pamoja na alama mara baada ya kutunga swali. Hivyo, hii ni hatua muhimu mara baada ya kutunga swali.

### 7.1 Mambo ya Kuzingatia Katika Kuandaa Mwongozo wa Usahihishaji

Wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa:

(a) Jibu liandikwe mara baada ya kutunga swali husika ili kuepuka kusahau jibu sahihi kwa swali lililotungwa.

Hatua hii itasaidia kufahamu jibu zuri na uzito wa alama kwa jibu la swali husika. Iwapo kutakuwa na ugumu katika kubainisha jibu sahihi ni ishara kuwa hata wanafunzi watapata wakati mgumu katika kujibu swali hilo. Hivyo uandaaji wa majibu utatoa nafasi kwa mwalimu kurekebisha maswali na kutengeneza mwongozo wenye kukidhi mahitaji ya kila swali katika usahihishaji.

- (b) Mwongozo wa usahihishaji uwe mkamilifu, unaoeleweka na kuweza kutumika na walimu wa somo husika au wasiokuwa wa somo husika katika usahihishaji wa mtihani/jaribio la somo husika. Hatua hii itasaidia kuufanya mwongozo huo kuwa na manufaa zaidi kwa walimu kwani wataweza kuuelewa kwa urahisi.
- (c) Mwongozo wa usahihishaji ufanyiwe majaribio. Waoneshe walimu/wasahihishaji wengine mwongozo huo ili waweze kubaini uthabiti na udhaifu katika majibu ya maswali ya jaribio husika. Katika hatua hii chagua sampuli ndogo ya majibu ya wanafunzi na kuyasahihisha kwa lengo la kubaini usahihi wa mwongozo wenyewe. Ikiwa itabainika dosari yoyote maboresho yafanyike kabla ya kuanza kuutumia.
- (d) Mgawanyo wa alama uzingatie uzito wa matakwa ya swali (task), hususan kile anachotakiwa kukifanya mwanafunzi ili kujibu swali husika.

## **8.0 UREKEBISHAJI WA MASWALI YA UPIMAJI/MITIHANI**

Urekebishaji wa maswali ya upimaji/mtihani ni kitendo kinachohusisha michakato ya kuthibiti ubora wa maswali ya upimaji kwa kutumia wataalamu wa elimu katika kuhakikisha yanalenga kutenda haki (fair), yanaaminika (valid), kuthibitika (reliable) na

yameandaliwa kwa kuzingatia viwango stahiki. Katika ngazi ya shule Jopo la Urekebishaji linaweza kuundwa na walimu wazoefu wanaofundisha somo husika kwa kushirikiana na ofisi ya taaluma. Zana muhimu zinazohitajika wakati wa urekebishaji ni pamoja na maswali yanayotakiwa kurekebishwa, mwongozo wa usahihishaji, muhtasari, kamusi, jedwali la utahini na vitabu vyatireka (vitabu vyatireka na kiada).

Ni muhimu kufanya urekebishaji wa maswali ya mtihani kabla ya kufanyika ili kupunguza dosari mbalimbali zinazoweza kuleta changamoto katika ufanyikaji. Changamoto hizo ni kama vile: maswali kutokuwa na matakwa yaliyo bayana, uzito usiostahili ukilinganishwa na matakwa ya swali, matumizi ya maneno yenye utata, maswali kuwa na majibu mengi, makosa ya kitahajia, kisarufi na kimundo na kutozingatia muhtasari unaotumika.

Katika ngazi ya shule urekebishaji huweza kufanywa na jopo la walimu wanaofundisha somo husika wakishirikiana na ofisi ya taaluma. Wakati wa urekebishaji, wahusika wanapaswa kuhakiki yafuatayo:

- (a) Ubayana, urefu na muundo wa maswali.
- (b) Matumizi sahihi ya lugha katika maswali.
- (c) Tahajia sahihi katika maswali (uandishi sahihi wa maneno).
- (d) Uwepo wa mwongozo wa usahihishaji wenye kuakisi matakwa ya swali na alama zinazoshabihiana na uzito wa swali.
- (e) Uwepo wa fomula, jedwali au michoro katika maswali yanayohitaji vitu hivyo.
- (f) Uwepo wa maelekezo bayana ya swali husika.
- (g) Misamiati iliyotumika inaendana na ngazi ya wanafunzi wanaopimwa.
- (h) Muda wa upimaji uliowekwa unaendana na urefu/ugumu wa upimaji.

## **9.0 UENDESHAJI WA UPIMAJI**

Uendeshaji wa upimaji ni kazi zote zinazojumuisha usambazaji au ugawaji wa upimaji, usimamizi na ufanyikaji wake. Kazi hizi

zinawahusu wasimamizi na wafuatiliaji. Msimamizi wa upimaji katika mkondo atakuwa na majukumu kabla ya upimaji kufanyika, wakati wa upimaji kufanyika na baada ya upimaji kufanyika.

### **9.1 Majukumu ya Msimamizi Kabla ya Upimaji Kufanyika**

Kabla upimaji haujafanyika mwalimu anayehusika na usimamizi anapaswa kufanya mambo yafuatayo:

- (a) Afike katika chumba cha upimaji atakachosimamia na kukikagua ili kuhakikisha kuwa:
  - (i) Meza na viti ni safi na havina maandishi yoyote.
  - (ii) Meza zimepangwa kwa umbali wa mita moja au zaidi kati ya meza moja na nyingine.
  - (iii) Madawati yamepangwa kwa kufuata alfabeti za herufi za kwanza za majina ya wanafunzi.
  - (iv) Kuta za ndani na nje ya chumba cha upimaji/mtihani hazina maandishi yoyote. Iwapo kuna michoro ya kudumu kama vile ramani, ahakikishe inafunikwa kabisa kwa kutumia karatasi au vitambaa visivyopitisha mwanga.
  - (v) Chumba ni safi na hakuna kitu chochote kisichoruhusiwa ndani ya chumba cha upimaji.
  - (vi) Vyoo vinavyotumiwa na wanafunzi ni safi na havina maandishi yoyote.
- (b) Anawaita wanafunzi karibu na chumba cha upimaji, kuwatangazia kwamba hawaruhusiwi kuingia ndani ya chumba na kitu kisichoruhusiwa na tukio lolote la udanganyifu litawafanya wafutiwe matokeo yao yote na kuadhibiwa kwa mujibu wa kanuni na sheria za shule.
- (c) Kuwapekua wanafunzi kabla hawaingia ndani ya chumba cha upimaji na kuhakikisha kuwa, hawaingii ndani ya chumba cha upimaji wakiwa na kitu chochote kisichoruhusiwa.

## **9.2 Majukumu ya Msimamizi Wakati wa Ufanyikaji wa Upimaji**

Wakati wa ufanyikaji wa upimaji msimamizi atatakiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (a) Kuwaruhusu wanafunzi waingie ndani ya chumba cha upimaji nusu saa kabla ya upimaji kuanza kufanyika na kuhakikisha kila mwanafunzi amekaa katika kitie chake.
- (b) Kufungua bahasha za maswali.
- (c) Kugawa karatasi za maswali kwa kila mwanafunzi na kuhakikisha kila mwanafunzi anapata karatasi moja tu ya maswali.
- (d) Kuwaruhusu wanafunzi kujaza taarifa zao katika karatasi za kujibia na kuhakikisha kila mwanafunzi anaandika jina lake au kuandika/kusiliba namba yake ya upimaji kwa usahihi.
- (e) Kuruhusu upimaji kuanza na kuwajulisha wanafunzi muda watakaomiliza kufanya upimaji.
- (f) Kuhakikisha katika muda wote wa upimaji kufanyika, kamwe chumba cha upimaji hakiachwi bila ya kuwa na msimamizi.
- (g) Kuhakikisha kuwa, kila mwanafunzi anafanya kazi yake mwenyewe na wanafunzi hawatazamiani au kusaidiana kwa namna yoyote ile.
- (h) Kusimamia ufanyikaji wa upimaji na kuhakikisha kuwa kwa muda wote anawaona wanafunzi wote kwa pamoja.
- (i) Kuhakikisha kuwa mwanafunzi au mtu ye yeyote hatoi karatasi ya maswali nje ya chumba cha upimaji wakati upimaji ukiendelea.
- (j) Kuhakikisha mwanafunzi anapolazimika kwenda kujisaidia, anapekuliwa kabla ya kutoka nje na

anaporejea, anapekuliwa tena kabla ya kuingia katika chumba cha upimaji.

- (k) Iwapo anasimamia wanafunzi wenyе mahitaji maalum, ahakikishe anawaongezea muda wa ziada kwa dakika 10 kwa kila saa moja ya upimaji kwa masomo yote isipokuwa somo la Hisabati waongezewe dakika 20 kwa kila saa.
- (l) Iwapo anasimamia wanafunzi wenyе ulemavu wa viungo wenyе uthibitisho kuwa unaweza kuwaathiri katika kuandika upimaji, ahakikishe anawaongezea muda wa ziada sawa na wanafunzi wasioona.
- (m) Kufuatilia kwa karibu mwenendo wa wanafunzi wakati wote wa ufanyakaji upimaji na kuhakikisha kuwa hakuna wanafunzi:
  - (i) wanaowasiliana ndani ya chumba cha upimaji,
  - (ii) wanaobadilishana karatasi za kujibia;
  - (iii) wanaotazamiana kazi zao; na
  - (iv) wanaonakili majibu kutoka kwenye vikaratasi walivyokuwa wameficha ambavyo havikubainika wakati wa upekuzi.
- (n) Kuhakikisha kuwa wanafunzi hawaruhusiwi kuondoka kwenye chumba cha upimaji nusu saa kabla ya muda wa upimaji kumalizika ili kuweza kufuatilia vizuri ukusanyaji wa karatasi za majibu.
- (o) Kuhakikisha kuwa mwanafunzi anayemaliza kufanya upimaji baada ya saa moja kupita tangu kuanza kwa upimaji na kuomba kutoka nje ya chumba cha upimaji anakabidhi karatasi ya majibu yake na karatasi ya maswali kabla ya kuruhusiwa.

### **9.3 Majukumu ya Msimamizi Baada ya Upimaji Kufanyika**

Msimamizi atatakiwa kufanya yafuatayo:

- (a) Kukusanya karatasi zote za majibu za wanafunzi kwa kufuata mtiririko wa majina yao kwa alfabeti za herufi za

kwanza za majina kuanzia A hadi Z au namba zao za upimaji na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi ameandika jina au kuandika/kusilia namba yake.

- (b) Kuhesabu karatasi zote za majibu ili kuhakikisha kuwa idadi ya wanafunzi waliofanya upimaji ni sawa na idadi ya karatasi zilizokusanywa.
- (c) Kupanga karatasi za majibu kwa kufuata alfabeti za herufi za kwanza au namba za wanafunzi, za mwanzo juu na za mwisho chini na kuziingiza ndani ya bahasha ya kurudishia majibu.

## 10.0 USAHIHISHAJI WA UPIMAJI

Usahihishaji wa upimaji ni zoezi linalofuata baada ya usimamizi na ufanyikaji wa mtihani/jaribio. Zoezi hili ni muhimu katika kutoa tathmini ya walichojobu wanafunzi. Usahihishaji wa mtihani/jaribio unatakiwa kufanyika kwa haki na usawa wa hali ya juu. Jopo la usahihishaji linatakiwa lihakikishe kila msahihishaji anasahihisha swali moja kutoka kwenye karatasi ya majibu ya mwanafunzi. Hii itasaidia kutenda haki na kuondoa uwezekano wa kumwonea au kumpendelea mwanafunzi yejote. Ili kuhakikisha usahihi wa usahihishaji na utoaji wa alama, wahakiki wanatakiwa kuteuliwa ili kuhakikisha kila swali limesahihishwa kwa kuzingatia mwongozo wa usahihishaji na alama za kila swali na alama za jumla za kila mwanafunzi zimetolewa kwa usahihi.

Endapo kutakuwa na mwalimu mmoja wa somo, uongozi wa shule unaweza kuwashirikisha walimu wa shule ya jirani katika kuunda jopo la usahihishaji. Endapo hakutakuwa na shule ya jirani ili kupata walimu wa kuunda jopo, mwalimu wa somo atasahihisha karatasi za wanafunzi na walimu wa masomo yanayoshabihiana wanaweza kutumika katika kufanya uhakiki wa usahihishaji kwa kutumia mwongozo wa usahihishaji uliosanifiwa ambao umeandaliwa na mwalimu wa somo. Wahakiki watahakikisha kuwa usahihishaji kwa kila karatasi ya majibu ya mwanafunzi umefanyika kwa kuhakikisha:

- (i) Kila swali limesahihishwa katika karatasi ya majibu na taratibu zote za usahihishaji zimefuatwa;
- (ii) Alama za pata (✓) au kosa (x) zimetumika mahali panapostahili;
- (iii) Utoaji wa alama umefuata mwongozo wa usahihishaji; na
- (iv) Uhamishaji wa alama kutoka kwenye karatasi ya mwanafunzi kwenda kwenye karatasi ya kurekodia alama umefanyika kwa usahihi.

Iwapo upimaji utafanyika katika ngazi ya Halmashauri, Mkoa au Taifa jopo la usahihishaji litaundwa na mamlaka husika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa ambavyo ni pamoja na kuwa na mwalimu mtaalamu wa somo husika na taaluma inayoendana na ngazi husika ya wanafunzi.

## **11.0 KUREKODI ALAMA ZA UPIMAJI**

Alama za wanafunzi hurekodiwa kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

- (a) Kuingizaji alama katika fomu maalum ya kunasa alama. Kila mwalimu wa somo atajaza alama za majoribio za kila mwanafunzi kwenye fomu maalum iliyoadaliwa na shule.
- (b) Kuhakiki alama katika fomu maalum za kurekodi alama. Taarifa za alama za darasa husika baada ya kuingizwa kwenye fomu maalum ni muhimu zikahakikiwa. Uhakiki utafanyika kwa kutumia alama zilizoko katika katarasi ya jaribio ya mwanafunzi kwa somo husika. Aidha, anayehakiki anatakiwa kuhakikisha kuwa, jina au namba ya mwanafunzi husika vimeandikwa kwa usahihi na alama alizopata mtahiniwa kwa kila swali zimerekodiwa kwa usahihi.
- (c) Kuhamishia alama katika kadi za maendeleo. Wastani wa alama za mwanafunzi zilizoingizwa kwenye taarifa za alama zilizochapwa za upimaji kwa mihula yote ya mwaka zihamishiwe katika kadi ya maendeleo ya kila mwanafunzi kwa matumizi ya Baraza la Mitihani la Tanzania.

## **12.0 UPIMAJI WA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM**



Upimaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum ni vema uzingatie aina ya ulemavu wa mwanafunzi husika. Kwa upande wa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo upimaji wao na usimamizi utategemea aina na namna ulemavu wao ulivyo pamoja na mahitaji yanayotakiwa. Kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuandika vizuri kutokana na ulemavu walionao wanapewa maswali yanayohitaji majibu mafupi (Objective Questions) na wanafunzi wasioweza kuandika kabisa watajibu maswali ya upimaji kwa mdomo na majibu yao yataandikwa na msimamizi au mwalimu aliyepewa dhamana hiyo.



Aidha, wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia wanafanya upimaji sawa na wanafunzi wa kawaida isipokuwa wanaongezewa muda wa dakika 10 kwa kila saa katika masomo yote na dakika 20 kwa somo la Hisabati. Msimamizi wa wanafunzi hawa anatakiwa kuwa mtaalamu wa lugha ya alama kwa ajili ya kufafanua maelekezo.

Kwa upande mwingine, upimaji wa wanafunzi wasioona unatakiwa kuandikwa kwa kutumia maandishi ya nukta nundu (Braille). Endapo maswali yanahusisha ramani au michoro yanatakiwa yabadilishwe kuwa katika maneno. Aidha, upimaji wa wanafunzi wenye uoni hafifu maandishi yao yanatakiwa kukuzwa ili yasomeke kwa urahisi. Kwa kutegemeana na aina ya ulemavu alionao mwanafunzi, mtahini anatakiwa kuwapa wanafunzi muda wa ziada wa dakika 10 kwa kila saa katika masomo yote isipokuwa katika somo la Hisabati ambapo watatakiwa kuongezewa dakika 20 kwa kila saa. Mifano ya maswali yaliyoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi wasioona imebainishwa katika Jedwali Na. 8.

## Jedwali Na 8: Mfano wa Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Wanafunzi Wasioona

Maswali ya Wanafunzi Wasio na Ulemavu							Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Maswali ya Wanafunzi Wasioona																					
1. Tabu alitembelea kituo cha hali ya hewa kilichopo uwanja wa ndege wa Mwanza kuchukua takwimu za hali ya hewa ya eneo hilo, na kuwasilisha takwimu hizo katika Jedwali kama ifuatavyo:							1. Tabu alitembelea kituo cha hali ya hewa kilichopo uwanja wa ndege wa Mwanza kuchukua takwimu za hali ya hewa zilizorekodiwa kila siku kwa muda wa miaka 30. Takwimu hizo zilikuwa na wastani wa joto la nyuzi 18 na mvua isiyopungua mm 60 hadi mm 2000 au zaidi.																					
<table border="1" style="width: 100%; border-collapse: collapse;"> <thead> <tr> <th>Mwezi</th><th>J</th><th>F</th><th>M</th><th>A</th><th>M</th><th>J</th></tr> </thead> <tbody> <tr> <td>Mvua (mm)</td><td>8 0 0</td><td>80 0 0</td><td>100 0 0</td><td>120 0 0</td><td>100 0 0</td><td>80 0 0</td></tr> <tr> <td>Jotoridi (°C)</td><td>1 8</td><td>18</td><td>24</td><td>28</td><td>24</td><td>18</td></tr> </tbody> </table>							Mwezi	J	F	M	A	M	J	Mvua (mm)	8 0 0	80 0 0	100 0 0	120 0 0	100 0 0	80 0 0	Jotoridi (°C)	1 8	18	24	28	24	18	(a) Takwimu alizoziona katika kituo hicho huitwaje?  (b) Ni aina ipi ya tabia nchi inawakilishwa na taarifa hizi?
Mwezi	J	F	M	A	M	J																						
Mvua (mm)	8 0 0	80 0 0	100 0 0	120 0 0	100 0 0	80 0 0																						
Jotoridi (°C)	1 8	18	24	28	24	18																						
<p>(a) Ni mwezi upi ulikuwa na mvua na jotoridi kubwa?</p> <p>(b) Ni aina ipi ya tabia ya nchi inawakilishwa na taarifa zilizopo kwenye jedwali?</p> <p style="text-align: center;"><b>(Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi)</b></p>																												
2. Jamali alipewa picha ya umbo la pembe tano lenye ukubwa wa pembe kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 1.							2. Jamali alipewa picha ya umbo la pembe tano lenye ukubwa wa pembe $120^\circ$ -y, $3y+100^\circ$ , $y+60^\circ$ , $5y+140^\circ$ na $2y-80^\circ$ . Kama mtaalamu wa Hisabati, ipi katika																					

Maswali ya Wanafunzi Wasio na Ulemavu	Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Maswali ya Wanafunzi Wasioona
 <p>Kielelezo Na 1.</p> <p>Kama mtaalamu wa Hisabati, ipi kati ya zifuatazo ni thamani ya <math>y</math>?</p> <p>A 2      B 20      C 4      D 38      E 88</p> <p><b>(Hisabati)</b></p>	<p>ya zifuatazo ni thamani ya <math>y</math>?</p> <p>A 2      B 20      C 4      D 38      E 88</p>
<p>3. Juma alipewa kazi ya kujenga banda la kuku na akalijenga kama linavyoonekana katika umbo lifuatalo:</p> 	<p>3. Umbo lenye pande tatu zinazolingana linaitwaje?</p> <p>A Pembetatu pacha      B Pembetatu mraba      C Pembetatu sawa      D Pembetatu guni      E Pembetatu sambamba</p>
<p>Kama mtaalamu wa maumbo ya kihisabati, umbo hili linaitwaje?</p> <p>A Pembetatu pacha      B Pembetatu mraba      C Pembetatu sawa      D Pembetatu guni      E Pembetatu sambamba</p> <p><b>(Hisabati)</b></p>	

Maswali ya Wanafunzi Wasio na Ulemavu	Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Maswali ya Wanafunzi Wasioona						
<p>4. Ikiwa eneo la trapeza ABCD ni <math>\text{sm}^2</math> 160, upi ni urefu wa BE?</p>  <p>A    sm 8              B    sm 10      C    sm 5              D    sm 20      E    sm 13</p> <p><b>(Hisabati)</b></p>	<p>4. Urefu wa pande sambamba za trapeza ni sm 12 na sm 20. Ikiwa eneo la trapeza ABCD ni <math>\text{sm}^2</math> 160, tafuta kimo cha trapeza hiyo.</p> <table> <tr> <td>A    sm 8</td> <td>B    sm 10</td> </tr> <tr> <td>C    sm 5</td> <td>D    sm 20</td> </tr> <tr> <td>E    sm 13</td> <td></td> </tr> </table>	A    sm 8	B    sm 10	C    sm 5	D    sm 20	E    sm 13	
A    sm 8	B    sm 10						
C    sm 5	D    sm 20						
E    sm 13							
<p>5. Kijiji cha Mtakuja kilitaka kujenga zahanati katika kiwanja kinachowakilishwa na umbo lifuatalo:</p>  <p>Je, kiwanja hicho kina eneo kiasi gani katika meta za mraba? <b>(Hisabati)</b></p>	<p>5. Kijiji cha Mtakuja kilitaka kujenga zahanati katika kiwanja kinachoundwa na mistatili miwili ; wenye urefu wa sm 15 na upana wa sm 9 na wenye urefu wa sm 10 na upana sm 8. Je, kiwanja hicho kina jumla ya eneo kiasi gani katika meta za mraba?</p>						

Maswali ya Wanafunzi Wasio na Ulemavu	Maswali Yaliorekebishwa kwa Ajili ya Maswali ya Wanafunzi Wasioona																																			
<p>6. Chunguza Kielelezo kifuatacho kinachohusu mabadiliko ya kiumbo ya maji kisha jibu swali linalofuata.</p> <p>Kwa kutumia herufi A hadi D, bainisha mchakato unaosababisha mabadiliko ya hali moja kwenda nyingine kama mshale unavyoelekeza.</p> <p><b>(Sayansi na Teknolojia)</b></p> <p>7. Shule ya Msingi Chechemea iliandaa mahitaji ya vifaa vyaa kieletroniki vinavyohitajika pamoja na gharama zake kama inavyoonekana katika mkekakazi ufuatao:</p> <table border="1"> <thead> <tr> <th></th> <th>A</th> <th>B</th> <th>C</th> <th>D</th> </tr> <tr> <th>1</th> <th>Namb a</th> <th>Jina la Kifaa</th> <th>Idadi</th> <th>Gharama (Tsh)</th> </tr> </thead> <tbody> <tr> <td>2</td> <td>1.</td> <td>Televisheni</td> <td>1</td> <td>300,000</td> </tr> <tr> <td>3</td> <td>2.</td> <td>Tarakilishi</td> <td>2</td> <td>800,000</td> </tr> <tr> <td>4</td> <td>3.</td> <td>King'amuzi</td> <td>1</td> <td>90,000</td> </tr> <tr> <td>5</td> <td>4.</td> <td>Printa</td> <td>1</td> <td>250,000</td> </tr> <tr> <td colspan="3"><b>Jumla</b></td><td></td><td><b>1,440,000</b></td></tr> </tbody> </table> <p>Chunguza mkekakazi huo na kisha jibu maswali yafuatayo:</p> <p>(a) Kifaa chenye jina la “tarakilishi” kipo katika seli gani?</p> <p>(b) Je, utatumia fomula gani kupata jumla ya gharama za vifaa vyote?</p> <p><b>(Sayansi na Teknolojia)</b></p>		A	B	C	D	1	Namb a	Jina la Kifaa	Idadi	Gharama (Tsh)	2	1.	Televisheni	1	300,000	3	2.	Tarakilishi	2	800,000	4	3.	King'amuzi	1	90,000	5	4.	Printa	1	250,000	<b>Jumla</b>				<b>1,440,000</b>	<p>6. Ni mchakato upi husababisha mabadiliko ya kiumbo katika hali za maada zifuatazo?</p> <p>(a) Yabisi kuwa kimiminika.      (b) Kimiminika kuwa gesi.      (c) Kimiminika kuwa yabisi.      (d) Gesi kuwa kimiminika.</p> <p>7. Mwalimu wa Darasa la Pili alitaka kuandaa matokeo ya mtihani kwa kutumia program ya tarakilishi. Kama mwanafunzi mwenye uelewa juu ya tarakilishi;</p> <p>(a) Ni programu ipi ungeshauri kutumiwa na mwalimu?      (b) Kwa nini ni muhimu kutumia programu hiyo?</p>
	A	B	C	D																																
1	Namb a	Jina la Kifaa	Idadi	Gharama (Tsh)																																
2	1.	Televisheni	1	300,000																																
3	2.	Tarakilishi	2	800,000																																
4	3.	King'amuzi	1	90,000																																
5	4.	Printa	1	250,000																																
<b>Jumla</b>				<b>1,440,000</b>																																

### **13.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI**

Kazi ya kufuatilia na kutathmini mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji shuleni imekuwa kwa sehemu kubwa ikifanywa na Wathibiti Ubora wa Shule. Katika kutekeleza jukumu hilo, wamekuwa wakikagua maandalizi ya vifaa vyta mitaala kama vile; azimio la kazi, andalio la somo, nukuu za somo, shajara la somo, madaftari ya wanafunzi, majaribio na mazoezi wanayofanya wanafunzi. Aidha, hukagua mazingira ya shule kwa ujumla na kushauri ipasavyo.

Pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Wathibiti Ubora wa Shule, Baraza la Mitihani litaenedelea kufanya ufuatiliaji kuhusu tathmini na mchakato mzima wa upimaji shuleni kwa kushirikiana na Wathibiti Ubora wa Shule, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri na Walimu Wakuu. Lengo ni kumsaidia mwalimu kuboresha zaidi maswali yanayoandaliwa kwa ajili ya upimaji, zoezi la usahihishaji pamoja na mchakato mzima wa kurekodi na kutunza alama za matokeo ya upimaji ili kuwa na upimaji endelevu ulio bora.

Wathibiti Ubora wa Shule, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri na Walimu Wakuu watatumia orodha hakiki, karatasi za maswali, miongozo ya usahihishaji na taarifa za alama za wanafunzi katika kubaini ubora wa maswali yaliyotumika katika upimaji, zoezi la usahihishaji kama limezingatia utaratibu pamoja na usimamizi wa upimaji husika.

Aidha, katika Upimaji wa Tamati (Summative Assessment) Baraza la Mitihani litaendelea kufanya uchambuzi wa kila swali lililotumika katika upimaji. Uchambuzi utaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya wanafunzi wajibu maswali ya upimaji kwa usahihi na wengine kushindwa kujibu maswali hayo kwa usahihi. Lengo likiwa ni kutoa mrejesho kwa wadau wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji pamoja na upimaji katika ngazi ya shule.

## **14.0 HITIMISHO**

Upimaji bora ni ule unaozingatia taratibu zote stahiki na kutoa matokeo halisi yanayoendana na uwezo wa mwanafunzi husika. Baraza la Mitihani lina imani kuwa, kupertia mwongozo huu wadau wote wa elimu wakiwamo walimu wa shule za msingi pamoja na wathibiti ubora wa shule watatumia nafasi zao ipasavyo katika kuhakikisha kuwa mchakato mzima wa upimaji unafanyika kwa ufanisi mkubwa ili kuleta maendeleo ya taaluma kitaifa. Aidha, kila Mkuu wa Shule kama msimamizi mkuu wa taaluma katika shule yake atawajibika kuhakikisha kila mwalimu anazingatia mwongozo huu katika kuandaa maswali kwa ajili ya upimaji wa wanafunzi katika mitihani ya kila wiki, mwezi au muhula kwa lengo la kuinua kiwango cha elimu. Matokeo yatakayopatikana yatachangia upatikanaji wa wanafunzi wenyе umahiri wa kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari au kujunga na mafunzo ya vyuvo mbalimbali vyatati.

